
MINISTÈRE
DE L'INTÉRIEUR
*Liberté*
*Égalité*
*Fraternité*

WIZARA YA MAMBO YA NDANI

Idara ya wakaazi wa nchi za kigeni Ufaransa



# Mwongozo wa waomba hifadhi nchini Ufaransa

gDA septemba 2020

# MUHTASARI


1. Aina mbalimbali ya ulinzi........................................................................ 5

1.1. Hali ya mkimbizi ........................................................................................... 5

1.2. Ulinzi mbadala.............................................................................................. 5

2. Uanzilishi wa taratibu na uandikishaji wa ombi la hifadhi ............................6

2.1. Makaribisho ya kwanza ya waomba hifadhi. ..................................................... 6

2.2. Uandikishaji wa ombi la hifadhi katika kaunta ya ki pekee. ................................................. 7

2.2.1. Hatua ya kwanza : kuandikisha ombi lako la hifadhi katika ofisi ya wilaya._.................................... 7

■ Uamuzi wa Taifa lenye wajibu wa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi._............................................. 7

■ Kufuzu kwa ombi lako la hifadhi.......................................................................................... 8

■ Chaguo la lugha ya mahojiano kwa OFPRA ........................................................................... 9

■ Utoaji dhibitisho la ombi la hifadhi. ..................................................................................... 10

■ Uwezekano wa kuomba ruhusa ya kukaa nchini kwa sababu zisizo za hifadhi._................................. 11

2.2.2. Hatua ya pili: Uchunguzi mahitaji na kugharamiwa na OFII. ....................................................... 11

■ Kuzingatiwa kwa mahitaji yako ya kibinafsi katika kaunta ya ki pekee. ............................................... 12

■ Mapendekezo ya kugharamiwa ............................................................................................ 12

2.3. Mwongozo baada ya kupitia kwa kaunta ya ki pekee.................. 13

3. Masharti juu ya uchunguzi wa ombi la hifadhi........................................13

3.1. Uchunguzi na Ofisi ya Kifaransa ya kuhifadhi wakimbizi na wasio na Uraia rasmi (OFPRA). 13

■ Fomu ya OFPRA unayo paswa kujaza. .................................................................................. 14

■ Kutuma hati yako kwa OFPRA. ............................................................................................ 14

■ Thibitisho ya uanzilishi wa utaratibu wa ombi la hifadhi na OFPRA........................................... 15

■ Uchunguzi wa ombi lako kwa taratibu ya kawaida au kwa taratibu ya haraka. ............................... 15

■ Mahojiano ya kibinafsi na OFPRA. .......................................................................................16

■ Uchunguzi ya kimatibabu. .................................................................................................. 17

■ Maamuzi ya OFPRA. ......................................................................................................... 17

■ Kufanya rufaa dhidi ya maamuzi ya OFPRA............................................................................. 18

■ Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA. .................. 19

3.2. Uchunguzi na Mahakama ya kitaifa ya haki ya hifadhi (CNDA)........................................ 19

■ Muda wa rufaa. ................................................................................................................ 19

■ Msaada wa wakili. ............................................................................................................ 20

■ Kufanya rufaa. ................................................................................................................. 20

■ Thibitisho la pokezi wa rufaa. ............................................................................................. 21

■ Asili ya rufaa yenye kusababisha kusitisha maamuzi. ............................................................... 21

■ Usikilizaji wa kesi yako na CNDA. ......................................................................................... 22

■ Maamuzi ya CNDA............................................................................................................ 23

■ Tamati ya ruhusa ya kuendelea kukaa nchini kufuatia maamuzi ya CNDA. ........................................... 24

3.3. Kufunguliwa upya kwa ombi la hifadhi liliofungwa. ....................................................... 24

3.4. Uchunguzi upya. ................................................................................................ 25

4. Vifaa vya mapokezi ya muomba hifadhi na haki yake .............................27

**4.1. Kupewa malazi kwa muomba hifadhi. ... 27**
- Mahali pa malazi. ... 27
- Maelekezo kwenye malazi. ... 27
- Kuingia na kuondoka kwenye makazi. ... 28

**4.2. Msaada wa muomba hifadhi (ADA). ... 28**
- Masharti ya kunufaika na msaada huu ... 28
- Muundo wa ombi. ... 29
- Kiwango cha msaada. ... 29
- Malipo. ... 29
- Kufanya rufaa. ... 30

**4.3. Fursa ya kupata elimu. ... 30**

**4.4. Fursa ya kupata matibabu. ... 31**
- Jee, unaweza pata matibabu wapi? ... 31
- Jee, unawezaje nufaika na msaada wa kugharamia karo ya matibabu yako? ... 31

**4.5. Ushiriki katika soko la ajira. ... 32**

**5. Matokeo ya kukataliwa kwa ombi la hifadhi kuhusu haki yako ya kuendelea kukaa nchini ... 34**

**5.1. Maamuzi ya kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA au CNDA. ... 34**
- Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA. ... 34
- Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini kuanzia kusomwa au kuarifiwa juu ya maamuzi ya CNDA. 36

**5.2. Kusaidiwa kurudi kwa nchi yako ya asili. ... 37**

**5.3. Ugumu wa kurudi katika nchi yako ya uraia. ... 38**

**6. Haki ya wanao nufaika na hali ya ulinzi ... 39**

**6.1. Kuishi Ufaransa. ... 39**

**6.2. Kuishi kwa jamaa yako. ... 39**
- Haki ya kuishi kwa jamaa yako. ... 39
- Haki ya muungano wa kifamilia. ... 40

**6.3. Ushirikishwaji. ... 40**
- Sahihi ya mkataba wa ushirikiano ya kijamhuri na Afisi ya kifaransa ya uhamiaji na ushirikiano (OFII) ... 41

**6.4. Haki ya kijamii. ... 41**
- Kupata makazi. ... 41
- Kujiunga na soko la ajira. ... 41
- Kupata matibabu. ... 42
- Huduma ya kijamii na kifamilia. ... 42

**6.5. Safari ya ngambo. ... 43**

**6.6. Kupata uraia. ... 44**

**6.7. Tamati ya hali ya hifadhi. ... 44**

**KIAMBATANISHO: anwani muhimu ... 45**

**1. Anwani za kitaifa ... 45**
- Taasisi ... 45
- Shirika ya kimataifa ... 45
- Mashirika ... 46

**2. Anwani ya mitaa** ........ **47**
■ Kaunta za ki pekee ........ 47
■ Wilaya ........ 49
■ Ukurugenzi wa kieneo ya Ofisi ya Kifaransa ya uhamiaji na ushirikiano (OFII) 51

# 1. Aina mbali mbali ya ulinzi

Unapo salimisha ombi la hifadhi na kama uchunguzi wake unategemea ni jukumu ya Ufaransa, ombi lako lita timizwa na mamlaka ya ulinzi, Ofisi ya Kifaransa ya Ulinzi wa wakimbizi na wasio na uraia wowote (OFPRA), chini ya mapitio ya mahakama kuu ya kitaifa ya sheria ya wakimbizi (CNDA).

Baada ya kukamilisha uchunguzi wa ombi lako la hifadhi, maafisa wa ulinzi wanaweza kukutunukia ulinzi kwa hali ya hifadhi: aidha utambuliwe ki rasmi kama mkimbizi, aidha utafaidishwa na ulinzi mbadala.

## 1.1. Hali ya mkimbizi.

Unaweza tambuliwa ki rasmi kama mkimbizi kulingana na misingi mitatu:

- **Kongamano ya Geneva** kuhusu hali ya wakimbizi ya 28 julai 1951. Hali ya mkimbizi unakubaliwa "*kwa mtu yeyote ambaye(...) ana hofu halali ya kuteswa kwa ajili ya rangi, dini, uraia wake, kujumuika kwake na kikundi ya kijamii au maoni ya kisiasa, anaishi nje ya nchi yake ya uraia na hawezi au, kwa ajili ya hofu hii, hataki kuomba ulinzi wa nchi hii* » ;
- **Hifadhi unatambuliwa kuwa "ya kikatiba"**, iwapo ina chanzo chake katika ibara 4 ya utangulizi wa katiba ya 1946. Hali ya mkimbizi unakubaliwa kwa "mtu yeyote anayeteswa ka ajili ya tendo lake kwa manufaa ya uhuru" ;
- **Jukumu ya Shirika Kuu ya Umoja wa Mataifa ya Wakimbizi (HCR)**: iwapo ulitambuliwa kama mkimbizi na shirika la UNHCR, chini ya msingi wa ibara ya 6 na 7 ya amri yake.

## 1.2. Ulinzi mbadala.

Faida ya ulinzi mbadala unapewa kwa mtu yeyote asiye kamilisha mahitaji ya kutunukiwa hali ya mkimbizi lakini ambaye anakumbwa na sababu kubwa na dhabiti ya kulengwa, nchini kwake, na hatari ya ukweli ya kufanyiwa madhara makubwa yafuatayo:

- hukumu ya kifo au kunyongwa;
- mateso au adhabu au matibabu ya kikatili au ya kudunisha;
- kuhusiana na raia, tishio mkubwa na kibinafsi dhidi ya maisha au nafsi yake kwa ajili ya vita ambayo inaweza fanyiwa kwa watu bila kujali hali yao ya kibinafsi na inayoweza sababisha hali ya vita ya silaha ya kindani au ya kimataifa.

**Hali ya mtu asiyekuwa na uraia wowote**

Kulingana na kongamano ya New York ya 28 Septemba 1954 kuhusu watu wasio na uraia wowote, hali ya kutokuwa na uraia unaweza tunukiwa mtu yeyote "*ambaye hakuna nchi yoyote inayo mkubali kama mwenyeji wake kutumia sheria yake* ".

Hali hii ni tofauti na aina zingine mbili ya ulinzi iliyotajwa awali na haina uhusiano na kitendo cha ombi la hifadhi. Basi haupaswi kuwasiliana na wilaya, lakini unafaa kuwasiliana moja kwa moja na OFPRA, ambayo, baada ya uchunguzi wa ombi lako, itaweza kukutunukia hali hii, chini ya sheria ya mahakama ya utawala.

# 2. Uanzilishi wa taratibu na uandikishaji wa ombi la hifadhi

Ili uandikishwe ombi la hifadhi nchini Ufaransa, unatakiwa mwanzoni kuwasiliana na kituo cha kwanza cha makaribisho ya wakimbizi (SPADA), ambacho kita kujulisha kuhusu utaratibu wa kuomba hifadhi na itakupa tarehe ya kuenda kwa kaunta ya ki pekee ya waomba hifadhi inayotambulika kwenye eneo.

Kaunta ya ki pekee ina jukumu ya kuandikisha ombi lako, ya kuamua utaratibu unaokufaa, ya kukagua udhaifu wako na kukutunukia, chini ya masharti mengine, msaada wa vifaa vya makaribisho (malazi, na msaada wa kifedha iliyotengewa waomba hifadhi).

**Unaweza wasilisha ombi la hifadhi katika hali zipi za kuishi?**

Unaweza wasilisha ombi la hifadhi katika hali yoyote ya kuishi bila kujali hali yako ya kuishi kulingana na sheria, iwapo unaishi kihalali au laa. Sababu ya kuishi kwako Ufaransa katika hali isiyo halali sio kizuizi cha kufanya ombi la hifadhi.

Unahimizwa kuwasilisha ombi lako la hifadhi hima baada ya kuingia nchini Ufaransa, hata iwapo uliingia Ufaransa na visa iliyo halali. Ikiwa hautawasalisha ombi lako kwa muda wa siku 90 baada ya kuingia nchini Ufaransa, huenda ombi lako halitakubalika.

## 2.1. Makaribisho ya kwanza ya waomba hifadhi.

Kabla ya kuenda kwenye kaunta ya ki pekee ya waomba hifadhi (GUDA), unapaswa kupitia kwenye idara ya makaribisho ya kwanza ya waomba hifadhi (SPADA). Idara hizi za makaribisho ya kwanza, ya msingi zilizoko chini ya mashirika, wanaajibika na kukusaidia na hatua zako ili uweze kufikia taratibu ya ombi la hifadhi.

Watekelezaji wa makaribisho ya kwanza wana manufaa yafuatayo:

- kukupa fahamu ya maada ya utekelezaji wa ombi la hifadhi;
- kukujulisha, kufuatia maelezo ya hali yako, fomu ya maelezo inayopatikana katika tovuti ambayo itatumiwa kwa kusajili ombi lako la hifadhi;
- kuitisha tarehe ya mkutano kwenye kaunta ya ki pekee na kukupa barua ya kuthibitisha mkutano huo. Barua hii itakuashiria mahali, siku na saa ambayo unapaswa kujitokeza bila ku kosa kwenye kaunta ya ki pekee. Mkutano huu hufanyika kwa kawaida ikichelewa sana siku 3 baada ya kukutana na mtekelezaji. inaweza sukumwa hadi siku 10 ikiwaa mahudhurio yatakua mengi;
- kupiga picha ya kitambulisho utakao ulizwa kwenye kaunta ya ki pekee.

Makaratasi yako yatapitishwa kwenye kaunta ya ki pekee kwa jumla kwa njia ya teknologia.

<u>TAHADHARI</u> : Ni lazima uzingatie tarehe na saa ambayo imeandikwa kwenye barua ya kukuagiza mkutanoni. Ikiwa utachelewa, hauta ruhusiwa kufikisha ombi lako na utaombwa urudi upya kwa idara ya mapokezi wa kwanza ili kufanya upya ombi la mkutano wa kusajiliwa kwa ombi lako.

Kumbuka, SPADA wataajibika na kukupea makao ikiwa hautapata makao kwenye Kituo cha Kukaribisha Wakimbizi (CADA) au idara yoyote ile ya makao imara ya wakimbizi baada ya kujiandikisha

kwako kwenye kaunta ya ki pekee (tazama sehemu "Jinsi ya kuthibitisha makao yako?" katika sehemu ya 2.2.1).

## 2.2. Uandikishaji wa ombi la hifadhi katika kaunta ya ki pekee.

Ili uweze kuandikisha ombi lako la hifadhi, unapaswa upitie kaunta ya ki pekee, ilivyo ashiriwa katika barua ya kukuita kwa mkutano uliyopewa na SPADA (tazama 2.1.).

Kaunta ya ki pekee inajumlisha maajenti wa wilaya na maajenti wa Idara ya Ufaransa wa Uhamiaji na Ushirikishwaji (OFII), wanaojumuika kwa lengo mahususi ya kuhakikisha makaribisho yako.

Kuna kaunta za ki pekee 33 zinazopatikana ndani ya nchi kuu ya Ufaransa (Unaweza tazama orodha kwenye kiambatanisho).

Mkutano kwenye kaunta ya kipekee unatekelezwa kwa hatua mbili:

- hatua ya kwanza na ma ajenti wa wilaya, ili ku andikisha ombi lako la hifadhi(2.2.1);
- hatua ya pili na ma ajenti wa OFII ili kuthibitisha mahitaji yako maalum na kubainisha jinsi matakwa yako yata gharamiwa (2.2.2).

**Jee, unatakiwa kuwa na anwani ya posta ili kuandikisha ombi lako la hifadhi?**

Haihitajiki uwe na makazi (anwani ya posta) ili kuandikisha ombi lako la hifadhi.

Kwa kinyume, itahitajika wakati wa kufanywa upya kwa thibitisho lako la hifadhi (tazama mnara "utoaji wa thibitisho ya ombi la usajili rasmi kama mkimbizi" katika sehemu ya 2.2.1).

### 2.2.1. Hatua ya kwanza: kuandikisha ombi lako la hifadhi katika ofisi ya wilaya.

**Jee, umeandamana na watoto wako wasiohitimu umri ya watu wazima?**

Ikiwa wamekuandama, nao pia watatambuliwa kama waomba hifadhi na wataandikishwa kwenye thibitisho lako la ombi la hifadhi. Ikiwa wazazi wawili wanaomba kusajiliwa, watoto watasajiliwa kwenye thibitisho ya mama yao, anaye tambuliwa kama mzazi mhusika toka mwanzo hadi mwisho wa taratibu. Hati hii haithibitishi muundo wa familia yako ila ombi ya usajili inayotekelezwa.

#### ■ Uamuzi wa Taifa lenye wajibu wa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi.

Baada ya kuthibitisha taarifa kamili iliyowasilishwa kwa kaunta ya kipekee na idara ya makaribisho ya kwanza, ajenti wa wilaya ata thibitisha kama nchi ya Ufaransa una jukumu la uchunguzi wa ombi lako.

Juu ya hayo, kwa kuwa umehitimu umri wa miaka 14 au zaidi, utachukuliwa alama ya vidole na ufanyishwe mahojiano ya kipekee yenye lengo la kufuatilia maisha yako toka nchi yako, na kuthibitisha ikiwa unaweza kuwa na jamii katika mataifa mengine waliopo katika muungano.

Ni chini ya ujumla wa mambo haya ambapo utateuliwa nchi iliyo na jukumu la kuamua ombi lako kwa kutumia sheria nambari °604/2013 ya bunge la Uropa na halmashauri ya 26 juni 2013, iitwayo sheria ya Dublin III.

**Nchi zinazohusika na mpangiio wa Dublin III**

Inahusu nchi 28 za Umoja wa bara  la Ulaya: Ujerumani, Austria, Ubeljiji, Bulgaria, Kroeshia, Kupro, Udenmarki*, Uhispania, Estonia, Ufinlandi, Ufaransa, Ugiriki, Hungaria, Uayalandi, Italia, Latvia, Lituanya, Luxemburg, Malta, Uholanzi, Poland, Ureno, Ucheki, Romania, Uingereza, Slovakia, Slovenia na Uswidi pamoja na nchi zingine nne wahusika:Iceland, Norwei, Uswisi na Liechtenstein.

* Udenmarki haitumii sheria ya "Dublin III", ingawaje wanazidi kutumia mapatano ya Dublin, iliyosahihishwa 15 juni 1990.

**Kwa uhakika, kuna uwezekano kwamba taifa nyingine ya Ulaya iwe na jukumu ya kuchunguza ombi lako la hifadhi badala ya Ufaransa, kwa mfano:**

- Ikiwa nchi nyingine ilikupa kibali cha makaazi au visa iliyo halali;
- Ikibainiki kwamba ulivuka mpaka wa nchi nyingine kinyume cha sheria kwa njia ya nchi kavu au anga au bahari;
- Ikiwa uliingia katika teritoria ya Umoja wa Ulaya kwa kupitia kwanza mipaka ya nchi husika iliyokupa visa;
- ikiwa ulisha andikisha ombi la hifadhi  katika nchi husika nyingine.

**Jee, kuna uwezo kwamba uchunguzi wa ombi lako la hifadhi iwe jukumu la nchi nyingine husika?**

Taratibu iitwayo "Dublin III" utatumika.  Basi ofisi ya wilaya itachukua jukumu ya kuwasiliana na nchi husika ili kuwaomba wakuhudumie.  Basi utapewa dhibitisho ya ombi la hifadhi, itakayo dumu kwa muda wa mwezi moja, kisha miezi nne na uwezo wa kufanywa upya, itakayo kuwezesha kukaa Ufaransa hadi uhamishwe katika nchi itakayokubali jukumu yako.

Uhamisho huu utapangwa na huduma ya wilaya ambayo itakujulisha maamuzi ya uhamiaji ikibainisha mfumo wa kuondoka kwako.  Una hadi muda wa siku 15 ili kupinga maamuzi haya mbele ya mahakama ya uraia.

## ■ Kufuzu kwa ombi lako la hifadhi.

**Ikiwa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi itakuwa jukumu ya Ufaransa,** OFPRA ndiyo shirika husika ya kuichunguza, iwe ni kwa mwendo wa kawaida au mwendo wa kuharakisha.  Kama ni taratibu ya kuharakisha, muda wa uchunguzi wa OFPRA hufupishwa, kwa kawaida siku kumi na tano lakini uhakikisho ni sawa katika miendo yote miwili.

- **Ombi lako litatekelezwa moja kwa moja kwa taratibu ya haraka,** kuanzia kaunta ya ki pekee, chini ya kesi mbili zifuatazo:
    - Ikiwa una uraia wa nchi inayo zingatiwa kama nchi ya asili kwenye (orodha ya nchi zinazo patikana katika ofisi ya wilaya au kwenye tovuti  ya OFPRA) ;
    - Ikiwa ulifanya ombi la kwanza la hifadhi ambalo lilikataliwa kwa kikamilifu na ukaomba kuchunguzwa upya kwa ombi lako.

- **Ombi lako lina weza tekelezwa kwa haraka**, kuanzia kaunta ya ki pekee, chini ya sababu zifuatazo:
  - Ukikataa kuchukuliwa alama za vidole;
  - Ikiwa unataka kuelekeza maafisa kufanya makosa kwa kuwaonyesha makaratasi zisizo halali, kwa kuwapa ishara zisizo za ukweli au kuficha mambo mengine ;
  - Ikiwa uliandikisha ombi kadhaa chini ya vitambulisho tofauti;
  - ikiwa ulichelewa kuandikisha ombi la hifadhi baada ya kuingia nchini Ufaransa (zaidi ya siku 90 na siku 60 nchini Guyana) ;
  - Ikiwa unaomba usajili ili kuharibu juhudi za kufukuzwa nchini;
  - Ikiwa uwepo nchini unachangia hatari kubwa kwa hali ya umma, usalama wa kitaifa au usawa wa Taifa.

OFPRA ina uwezo wa kurudisha ombi lililowekwa chini ya taratibu ya haraka wakati liliandikwa kuchunguzwa chini ya taratibu ya kawaida, isipokuwa kama ombi liliandikishwa kuchunguzwa chini ya mwendo wa haraka kwa sababu za usalama wa umma.

Ikiwa ombi lako litachunguzwa katika taratibu ya haraka, utapewa makala kadhaa ya kumbukumbu ya maelezo. Inafaa utume nakala moja kwa OFPRA wakati wa kuandikisha ombi lako, na nakala nyingine kwa CNDA, ikiwa utapinga maamuzi ya OFPRA kwenye mahakama.

**Kesi maalum: Jee, umelengwa na kitendo cha kufukuzwa au kupigwa marufuku ya kuishi nchini kwa maamuzi ya serikali au mahakama?**

Hata ikiwa umelengwa na juhudi kama hicho cha kufukuzwa nchini haimaanishi kwamba uzuiliwe kuandikisha ombi lako la hifadhi.

Ikiwa jukumu la uchunguzi wa ombi lako la hifadhi linakumba taifa ya Ufaransa, utaweza kupewa makao au uwekwe kizuizini.

Katika hali hii, OFPRA itachunguza ombi lako la hifadhi kwa muda uliyo fupishwa (saa 96) kufuatia kuwekwa kwako kwenye makao au kizuizini. Katika tukio la kukataliwa kwa uandikishaji wa ombi lako, haki yako ya kuendelea kuishi nchini Ufaransa itafika tamati. Unaweza, katika masaa 48, omba hakimu wa umma kutamatisha utekelezi wa kitendo cha kufukuzwa nchini wakati ambapo CNDA itachunguza malalamishi yako (tazama sehemu 5.1).

## ■ Chaguo la lugha ya mahojiano kwa OFPRA.

**Ikiwa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi itakuwa jukumu ya Ufaransa**, baada ya kuwasilisha ombi lako kwa OFPRA, isipokuwa katika swala la ki pekee, utafanyiwa mahojiano ya ki pekee na OFPRA.

Wakati wa kuandikisha ombi lako la hifadhi, unapaswa basi kuchagua lugha ambayo ungependa kuhojiwa nayo na OFPRA. Utapewa basi kumbukumbu ya kukuarifu juu ya lugha ambazo zinatumika katika mahojiano na OFPRA, ikiwa ni zaidi ya lugha 115. Hauruhusiwi kuibadilisha lugha ya mahojiano na ni lugha ulichagua ambacho kitatumika kukuhoji wakati wowote katika uchunguzi wa ombi lako la hifadhi.

Ikiwa haukuchagua lugha kati ya lugha zilizo tajwa katika kumbukumbu la maelezo, utahojiwa katika lugha ambacho una ufahamu ya kutosha.

Ikiwa utataka kupinga chaguo la lugha iliyotumika kukuhoji wakati wa taratibu yako ya ombi la hifadhi, hautaweza kuipinga ila kwa njia ya kufanya rufaa mahakamani mbele ya CNDA dhidi ya uamuzi wa OFPRA inayo amuru juu ya ombi lako la hifadhi.

TAHADHARI: Muda na aina ya mahojiano kwa OFPRA unahitaji zaidi ya ujuzi kinaga ubaga ya lugha. Ni sharti uelewe lugha ambayo unachagua na pia uweze kujieleza vizuri katika lugha hii.

### Utoaji wa dhibitisho la ombi la hifadhi.

Baada ya uamuzi wa nchi takayo kabithiwa jukumu ya ombi lako na kufuzu kwa taratibu ya ombi lako la hifadhi, utatunukiwa dhibitisho ya ombi la hifadhi.

**Ikiwa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi itaamuliwa kuwa jukumu la taifa nyingine shirika ya umoja wa bara la Uropa**, muda wa uhalali wa dhibitisho la ombi la kwanza ni mwezi moja. Itafanywa upya kwa muda wa miezi nne (tazama fungu la "Maamuzi ya taifa iliyo na jukumu ya uchunguzi wa ombi lako la hifadhi" katika sehemu 2.2.1).

**Iwapo uchunguzi wa ombi lako la hifadhi itaamuriwa kuwa jukumu la Ufaransa**, utatunukiwa dhibitisho la kwanza la ombi la hifadhi. Thibitisho hili ni la kudumu:

- kwa muda wa miezi kuma ikiwa ombi lako la hifadhi litachunguzwa chini ya utaratibu ya kawaida;

- kwa muda wa miezi sita ikiwa itachunguzwa chini ya utaratibu ya haraka.

Ofisi ya wilaya haiwezi kukukataza dhibitisho la ombi ya hifadhi ila kwa sababu zifuatazo:

- unaandikisha ombi mpya ya hifadhi baada ya kukataliwa awali kwa ombi la uchunguzi wa pili (tazama 3.4.) ;
- umelengwa na maamuzi kamili ya kupelekwa kwa nchi nyingine ambayo siyo nchi yako ya uraia ama kwamba umelengwa na maamuzi ya kukanusha hali yako kwa msingi ya mamlaka ya maamuzi ya sheria ya Ulaya au kwa msingi ya amri ya mahakama ya kimataifa ya makosa ya jinai.

Kwa muda wa siku 21 baada ya kutolewa kwa dhibitisho (siku 8 ikiwa ni ombi ya pili ya uchunguzi au kufungiliwa upya kwa kesi, tazama sehemu 3.3 na 3.4), unapaswa kutuma karatasi ya ombi la hifadhi, ambayo ulipewa na ofisi ya wilaya , kwa OFPRA (tazama 3.1 "Uchunguzi na OFPRA"). Ikiwa hati yako imekamilika, OFPRA watathibitisha kuipokea kwa kukuandikia barua.

Ili thibitisho lako la ombi la hifadhi liweze kufanywa upya, unapaswa kujiwasilisha katika afisi ya wiliya iliyoko mahali unapoishi. Thibitisho lako la ombi la hifadhi litafanywa upya kwa muda wa miezi sita, chini ya taratibu ya kawaida, vile vile chini ya taratibu ya haraka.

Kila utakapo fanya ombi la kufanyishwa upya kwa thibitisho la ombi lako, ili kukamilisha hati yako, unapaswa kuandama nyaraka za ushahidi zinazohitajika na wilaya, haswa zenye kuthibitisha anwani ya makazi yako. Ili kuthibitisha kwamba umefanya rufaa dhidi ya CNDA, unatakiwa kuwasilisha notisi ya mapokezi ya rufaa (tazama sehemu 3.2 "Uchunguzi na Mahakama ya kitaifa ya sheria ya uhifadhi").

**Jee, utaweza aje thibitisha makao yako?**

Kwa ombi za hifadhi zilizotekelezwa kuanzia tarehe 1 Januari 2019, unaweza thibitisha makao yako kwa njia zifuatazo:

-Kama umepewa malazi katika kituo cha waomba hifadhi au aina yoyote ya makazi dhabiti ya waomba hifadhi (ikitenga makao aina ya hoteli),kwa kuonyesha ushahidi wa makao;

-Ikiwa unaishi katika nyumba unayomiliki au uliokodisha au katika nyumba inayomilikiwa na mchumba wako/mtoto wako/jamii yako, kwa kuonyesha ushahidi wa makao;

Katika hali zingine, unatakiwa kuwa na malazi katika kituo cha mapokezi ya kwanza iliyokubaliwa na serikali kwa sababu za mapokezi na kuonyesha ushahidi wa makazi (tazama 2.1).

Kwa ombi za hifadhi zilizo andikishwa kabla ya tarehe 1 Januari 2019, unaweza kupata makao kulingana na maarifa zilizo tajwa hapo awali, lakini pia, ikilazimika, unaweza endelea kupata makao kwa mhusika wa tatu.

Thibitisho hili la ombi la hifadhi hufanywa upya wakati wowote, mradi uwe na ruhusa ya kuwa nchini kihalali. Kimsingi, una ruhusa ya kuwa nchini kihalali kwa wakati ambapo ombi lako la hifadhi lina chunguzwa, hadi wakati ambapo uta arifiwa kuhusu maamuzi ya OFPRA au, ikiwa utafanya rufaa mbele ya CNDA, hadi wakati ambapo uta arifiwa juu ya maamuzi wake, na ikilazimika, hadi kusomwa kwa maamuzi huu katika usikilizaji wa hadharani.

Hata hivyo, kuna uwezekano wa thibitisho lako la hifadhi kukanushwa au kukosa kufanywa upya, ikiwa:

- OFPRA ilikujulisha maamuzi ya kukataa au kutoweza kupokea ombi lako basi kutamatisha ruhusa yako ya kuwepo nchini kihalali (tazama 5.1 "Maamuzi ya kukataa kwa OFPRA au ya CNDA) ;
- Imejitokeza kwamba tarehe ya mwisho ya kufanya rufaa mbele ya CNDA haikuzingatiwa (tazama 3.2 "Uchunguzi na Mahakama ya kitaifa inayo shughulikia haki ya hifadhi").

<u>TAHADHARI</u>: Thibitisho ya ombi la hifadhi haikuruhusu kutembea wazi wazi kakita nchi nyinginezo katika Umoja wa Ulaya.

### ■ Uwezekano wa kuomba ruhusa ya kukaa nchini kwa sababu zisizo za hifadhi.

Ikiwa itaamuliwa kwamba ombi lako la hifadhi ni jukumu ya Ufaransa, utaarifiwa kwa uwezekano wa kuomba kibali cha makazi kwa sababu zisizo za hifadhi.

Utakabidhiwa notisi ya habari itakayo kujulisha wakati ambapo una weza fanya ombi hili. Muda huu ukisha pita, hautaweza kamwe kuwasilisha ombi la ruhusa ya kukaa nchini, ila kukiwa na hali mapya ya kuihalalisha.

## 2.2.2. Hatua ya pili: Uchunguzi wa mahitaji na kugharamiwa na OFII.

## Kuzingatiwa kwa mahitaji yako ya kibinafsi na kaunta ya ki pekee.

Wakati utapitia kaunta ya kipekee na baada ya kuandikisha ombi lako la hifadhi katika ofisi ya Wilaya, mhudumu wa OFII atakukaribisha kibinafsi ili kubaini mahitaji yako maalum kuhusu mapokezi.

Mahojiano yatafanyika kwa siri na haitazingatia sababu zako za kuomba hifadhi. Utaulizwa orodha ya maswali ili kuibainisha ikiwa una hitaji kupewa msaada mahususi ya mapokezi. Ikiwa hali yako itahitaji, mhudumu wa OFII atazingatia vipengele hizi ili kukuelekeza kwenye mahali pa malazi inayofaa.

Una haki ya kukubali au kukataa kujibu orodha ya maswali ya uchunguzi. Iwapo utakataa kujibu maswali, serikali haitakuwa na lawama ikiwa utaelekezwa katika makao ambayo haliambatani na mahitaji yako au kukosa kuarifiwa kwa OFPRA kuhusu hali yako.

Ikiwa utawasili nchini Ufaransa ukiwa na hati ya matibabu, ajenti wa OFII atawasilisha hati yako kwa siri kwa muuguzi wa OFII atakaye dhibitisha ikiwa hali yako inahitaji mapokezi iliyolinganishwa na mahitaji yako. Ikiwa unaugua, utaelekezwa kwenye kituo cha matibabu au huduma ya matibabu ya dharura ya hospitali iliyoko karibu.

Ikiwa ajenti wa OFII atagundua hali ya udhaifu kwako, kwa idhini yako, anaweza fahamisha OFPRA juu yake. Maelezo haya yana lengo la kuimarisha, kama ni lazima, masharti ya uchunguzi wa ombi lako la hifadhi na OFPRA (kwa mfano, kurahisisha mambo kwa faida ya watu walemavu, ama kuwepo wa mkalimani wa lugha ya ishara). Maboresho yanayofaa yatatathminiwa na OFPRA.

Mahitaji yanayohusika na hali ya udhaifu yanaweza zingatiwa katika muda wote wa uchunguzi wa ombi la hifadhi na wafanyikazi wa kijamii katika vituo vya malazi au vyama vinanyoajibika na kukupa mwongozo katika harakati zako za kiutawala na za kijamii.

## Mapendekezo ya kugharamiwa.

Wakati wa mkutano wako kwa kaunta maalum, OFII itakupa pendekezo ya kugharamiwa ambayo itakuwezesha kunufaika na msaada wa kifedha kwa muda wote wa kuruhusiwa kwako kukaa nchini kihalali kwa madhumuni ya ombi lako la hifadhi.

Hati ya pendekezo la kugharamiwa kwako utakayo pewa na OFII kwenye kaunta ya ki pekee inathibitisha muundo wa familia yako ili kubainisha kiwango cha haki unacho kulingana na msaada wa kifedha ya mapokezi utakaopewa. Hati hii ita haririwa upya na OFII iwapo mtoto atazaliwa au ataungana na wazazi wake katika kipindi cha utaratibu wa ombi la hifadhi ili kumueka kwenye hesabu ya haki ya kifedha ya mapokezi.

Kama ilivyoandikwa katika sehemu ya 4 ya mwongozo huu, msaada wa kifedha ya mapokezi yana kuwezesha:

- Ikiwa bado hauna makao na kuwa unaomba kugharamiwa, mahali pa makazi ambako utaelekezwa (tazama 4.1. " Kupewa malazi kwa muomba hifadhi "). ;
- isipokuwa katuka swala la ki pekee lililotengwa na sheria, kuhusu posho ya muomba hifadhi (tazama 4.2 "Msaada za muomba hifadhi").

Katika tukio la msongamano wa utaratibu wa mapokezi katika eneo fulani, OFII inaweza kukuelekeza katika eneo tofauti, ambako utahitajika kuishi wakati wa uchunguzi wa ombi lako (tazama 4.1 "Kupewa malazi kwa muomba hifadhi").

### 2.3. Mwongozo baada ya kupitia kwa kaunta ya ki pekee.

Baada ya kupitia kwenye kaunta ya ki pekee, utapendekezewa mwongozo katika mahali pako pa makazi, ikiwa inahusu kituo cha makaribisho kwa waomba hifadhi (CADA) au mahali pa makazi ya dharura inayo dhaminiwa kuwa imara (ambayo siyo hoteli).

Ikiwa haujapewa malazi kwa kituo kama hicho, mwongozo wako utahakikishwa na kituo cha SPADA ambako utaashiriwa na OFII (tazama sehemu 2.1).

Mwongozo huu aina ya kijamii, kisheria na kitawala inajumuisha bila shaka makazi (tazama kifungu "jinsi ya kuthibitisha makazi yako " katika sehemu ya 2.2.1) na ikiwa uchunguzi wa ombi lako la hifadhi ni jukumu ya taifa ya Ufaransa, usaidizi wa kuunda hati ya ombi la hifadhi inayotakiwa kuwasilisha katika OFPRA.

TAHADHARI : Ikiwa una makao SPADA, ni jukumu lako kuhakikisha kuwa unatafuta barua kila mara, ukizingatia maelekezo yaliyowekwa na SPADA

# 3. Masharti juu ya uchunguzi wa ombi la hifadhi

Ikiwa jukumu ya uchunguzi wa ombi lako la hifadhi itakuwa jukumu ya nchi ya Ufaransa, itachunguzwa na Ofisi ya Kifaransa ya kuhifadhi wakimbizi na wasio na uraia asili, chini ya uangalifu wa kisheria ya Mahakama ya kitaifa ya haki ya hifadhi.

## 3.1. Uchunguzi na Ofisi ya Kifaransa ya kuhifadhi wakimbizi na wasio na Uraia rasmi (OFPRA)

Wakati wa kuandikisha ombi lako la hifadhi, ofisi ya wilaya ilikupa fomu ya ombi la hifadhi ambayo unapaswa kujaza na kuwasilisha kwa OFPRA, ili iweze kuchunguzwa na kufanyiwa maamuzi.

Maamuzi ya OFPRA yanayo kataa ombi yanaweza kufanyiwa rufaa mbele ya CNDA (tazama 3.2. Uchunguzi wa ombi la hifadhi na Mahakama ya kitaifa ya haki ya wakimbizi).

Wakati wa kuwasilisha ombi lako la hifadhi, hautakiwi kuthibitisha aina ya hifadhi ambayo ungependelea (hali ya ukimbizi au hifadhi mbadala). Inahusu utaratibu ya ki pekee wakati ambapo ombi lako likachunguzwa na OFPRA, kwanza kwa mtazamo wa hali ya ukimbizi, kisha ikiwa hali yako haiambatani nayo, kwa mtazamo wa hifadhi mbadala.

## Fomu ya OFPRA unayo paswa kujaza.

**Fomu inapaswa kujazwa kwa lugha ya Kifaransa**, litiwe sahihi kisha iambatanishwe na thibitisho ya ombi la hifadhi iliyo halali, picha mbili ya kitambulisho na hati cha kusafiri unayo miliki**.**

Ikiwa ombi lako la hifadhi lilichukuliwa chini ya utaratibu wa haraka, unapaswa vile vile kuwasilisha nakala ya notisi ya habari uliopewa wakati wa kuandikisha ombi.

Ni lazima upeane hati hizi ndi posa ombi lako iandikishwe na OFPRA.

Ikiwa watoto wako wadogo wanaokuandama wamelengwa na hatari ya kibinafsi, unapaswa kuyaripoti katika fomu yako ya ombi la hifadhi. Ikiwa wazazi wote wawili ni waomba hifadhi, hatari zinazolenga watoto wadogo wanao waandama yataandikwa katika fomu ya mama mzazi.

Habari zinazopatikana katika ombi lako la hifadhi ni za siri na kwa wakati wowote hayatatolewa kwa serikali ya nchi yako ya asili.

## Kutuma hati yako kwa OFPRA.

Mara hati yako itakapo kamilika, **unapaswa kuituma, kuchelewa mno, siku ya 21** (siku ya 8 ikiwa ni ombi la kufunguliwa upya kwa kesi - tazama 3.3 Kufunguliwa upya kwa ombi la hifadhi iliyo tamatishwa - tazama 3.4 kuchunguza upya) ya kufuatia baada ya kupokea dhibitisho ya ombi ya hifadhi. Inapaswa kutumwa kwa njia ya posta pekee yake, kwa anwani ifuatayo:

OFPRA
201, rue Carnot
94 136 FONTENAY-SOUS-BOIS CEDEX

Kwa mfano, kama ulipokea thibitisho lako la ombi la hifadhi tarehe 10 Januari, unapaswa kuwa ulituma hati yako kwa OFPRA kuchelewa mno tarehe 31 Januari. Ni muhuri ya posta itakayo thibitisha.

Inapendekezwa sana utume hati yako kama "barua iliyosajiliwa yenye upokezi iliyosajiliwa", kwa kuandika jina yako kwa namna sahihi katika sehemu ya "mwandishi".

Ikiwa hati yako sio kamili, OFPRA ita irudisha kwako na kukupa siku 8 ya kuikamilisha na kuituma (siku 4 ikiwa ni ombi la kufunguliwa upya au kuchunguzwa upya kwa ombi). Ikiwa hauta tuma hati yako katika muda huu, OFPRA itatamatisha ombi lako la hifadhi, ruhusa yako ya kuishi nchini itatamatishwa na hautawezeshwa kufanya upya thibitisho lako la ombi la hifadhi.

Unaweza tumia OFPRA hati ya ziada wakati wowote kwa muda huu wa taratibu ya uchunguzi wa ombi lako. Unapaswa kuyahifadhi vyema nakala zote za barua unazozituma au kupokea kutoka kwa OFPRA, pamoja na thibitisho zote za kutuma au kupokea barua na posta. Kila utakapotuma barua kwa OFPRA,kumbuka kila wakati kuandika nambari ya hati yako iliyoko juu ya barua ya kuanzishwa kwa ombi lako la hifadhi uliyotumiwa na ofisi.

**Jee, umebadilisha anwani ya makazi wakati ambapo taratibu ya ombi inaendelea?**

Ikiwa ulifahamisha OFPRA anwani inayoambatana na mahali pako pa malazi, tofauti na anwani yako ya makazi, na ikiwa utabadilisha eneo la makazi, ni muhimu kujulisha OFPRA haraka iwezekanavyo,

imependekezwa ufanye hivyo kwa njia ya huduma ipatikanayo kwa sababu hii kwenye tovuti ya OFPRA (www.ofpra.gouv.fr), kifungu « *Utekelezaji kwa kutumia mtandao* ». Kwa hakika, OFPRA itazituma barua zako katika anwani iliyotumika kwa mara ya mwisho, sana sana barua ya mwito ya mahojiano au maamuzi iliyopitishwa juu ya ombi lako la hifadhi.

Ikiwa una makazi katika nyumba unayo miliki au kodisha au nyumba inayomilikiwa au kukodishwa na mchumba/mtoto/jamii yako, na ikiwa utabadilisha anwani, unapaswa kufahamisha OFII.

## Thibitisho ya uanzilishi wa utaratibu wa ombi la hifadhi na OFPRA.

Ikiwa hati yako imekamilika na imefikishwa kwa wakati unaofaa, OFPRA itakutumia barua ya kukufahamisha uanzilishi wa ombi lako ofisini mwake na kukupa nambari ya usajili ya hati yako.

Hati hii ni thibitisho rasmi kwamba ombi lako la hifadhi lilipokelewa vyema na OFPRA.

Ni hati hii ambayo itakuruhusu kufanya upya thibitisho lako la kwanza la ombi la hifadhi (tazama 2.2.1 "kutolewa kwa thibitisho ya ombi la hifadhi").

Mara nyingi, barua ya wito kwa mkutano hutumwa pamoja na barua ya uanzilishi wa uchunguzi wa ombi lako. Barua hii ya mwaliko kwa mkutano utakuwa kwenye mgongo wa barua ya uanzilishi. Ikiwa barua ya mwaliko kwa mkutano hauta andikwa kwenye mgongo wa barua ya uanzilishi, basi itatumwa baadaye kwa barua tofauti.

## Uchunguzi wa ombi lako kwa taratibu ya kawaida au kwa taratibu ya haraka.

Ombi lako la hifadhi litachunguzwa na OFPRA, aidha kwa taratibu ya kawaida, au kwa taratibu ya haraka.

Kama ilivyo ashiriwa katika sehemu 2.2.1 (kifungu "kufuzu kwa ombi lako la hifadhi"), muda wa uchunguzi katika taratibu ya haraka hufupishwa hadi siku 15 ingawaje utadhaminiwa kama inavyo fanywa chini ya taratibu ya kawaida. Hati yako itachunguzwa na OFPRA katika taratibu ya haraka ikiwa iliamuliwa hivyo wakati wa kuandikishwa kwa ombi lako la hifadhi katika kaunta ya ki pekee. Zaidi ya hapo, OFPRA ina ruhusa ya kubadilisha taratibu ya ombi lako na kuiweka kuwa taratibu ya kawaida ikiwa itathibitisha kuwa inastahili hivyo, baada ya uchunguzi wa hati yako au hali yako ya kibinafsi isipokuwa kama uwepo wako nchini unachangia hatari kuu kwa hali ya umma, usalama wa taifa au usawa wa taifa.

OFPRA inaweza pia amua kuchunguza kesi yako katika taratibu ya haraka chini ya kesi zifuatazo:

- ikiwa ulipeana makaratasi ya uongo, ulipeana ishara ya uongo au ulipeana ujumbe au makaratasi kwa nia ya kupotosha OFPRA;
- uliwasilisha ombi zingine za hifadhi chini ya vitambulisho tofauti;
- maswala uliyo ya simulia kuthibitisha haja yako ya hifadhi hayaambatani na mahitaji ya hifadhi;
- matamshi yako hayaeleweki, yanajipinga, yana dhihirika kua ya uongo au hayasadikiki na yanakanusha habari ambazo ofisi inamiliki kuhusu nchi yako ya asili.

Ikiwa ungependa kupinga kuwekwa kwa hati yako chini ya uchunguzi ya haraka, utaweza fanya hivyo kwa njia ya ki pekee ya kufanya rufaa mbele ya CNDA.

## Mahojiano ya kibinafsi na OFPRA

Punde OFPRA itakapo pokea ombi lako la hifadhi, utapokea barua ya mualiko kwa mahojiano.

Utaweza kukosa kufanya mahojiano chini ya hali mbili pekee:

- Ikiwa habari ulizodokeza katika hati yako yanatosha OFPRA kukutunukia hali ya mkimbizi;
- Iwapo sababu za kimatibabu, thabiti na zisizo za hiari yako, zinakuzuia kujitokeza na kushiriki katika mahojiano.

Ikiwa utapata barua inayokuita kwa mahojiano, unapaswa kujitokeza kwenye makao makuu ya OFPRA iliyoko Fontenay-sous-Bois. Hapo utahudumiwa na afisa wa OFPRA aitwaye "afisa wa hifadhi" kwa uwepo wa, ikiwa itatakikana, mkalimani aliyeajiriwa na OFPRA ambaye anazungumza lugha uliyochagua kwa kipindi cha kupitia kaunta ya ki pekee wakati wa kuandikisha ombi lako la hifadhi au kwa lugha ambayo una ufahamu ya kutosha (tazama kifungu "chaguo la lugha ya mahojiano kwa OFPRA sehemu ya 2.2.1). Unaweza omba wakati wowote kuhudumiwa katika lugha ya Kifaransa. Hauwezi kupinga lugha iliyotumiwa katika mahojiano hii ila kwa njia ya kufanya rufaa mbele ya CNDA.

**Ikiwa hautajitokeza katika mahojiano hii, kutokuwepo kwako kunaweza tuma OFPRA kufanya maamuzi juu ya ombi lako juu ya hati yako ama pia kuifunga**. Basi ni muhimu kuwa, iwapo utakuwa na kizuizi, ujulishe OFPRA angalau saa 48 mbeleni, au kuijulisha juu ya uwezekano wa kuchelewa, kwa kutumia anuani ya barua pepe iliyoko kwenye barua ya kukuitia mahojiano.

Ukipenda, unaweza fika kwa mahojiano ikiandamana na, aidha wakili, au msimamizi halali wa shirika inayotambuliwa na OFPRA ambayo itaweza kutoa maoni baada ya mahojiano. Hata hivyo, mahojiano hayata ahirishwa iwapo wakili au mwakilishi wa shirika hatakuwa wakati wa mahojiano. Ikiwa uko katika hali ya ulemavu, unaweza omba kuandamana na mhudumu wa afya anaye kushughulikia kwa kawaida au mwakilishi wa shirika ya usaidizi kwa watu ulemavu wakati wa mahojiano.

Ikiwa utapendelea kwamba mahojiano yafanywe na ajenti wa ofisi na/au mkalimani wa jinsia ya chaguo lako, kwa sababu za ugumu wa kuthibitisha sababu ya ombi lako, haswa sababu zinazo lingana na vurugu aina ya kingono, unaweza fanya ombi hili kwa OFPRA kabla ya siku ya mahojiano.

**Mahojiano yanafanyika kwa siri**. Matamko yako yatapatikana katika muhtasari itakayofanywa na afisa wa hifadhi aliyekuhoji na ukiulizia, utapewa maarifa juu yake kabla ya maamuzi kufanywa (katika taratibu ya kawaida) au ikichelewa mno uta yapata pamoja na maamuzi (katika taratibu ya haraka).

Bila shaka, mahojiano yanahusu kinasa sauti ambayo hautaweza kufikia ila kwa hali ya kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA na katika hali ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi huu.

**Jee unaweza hojiwa mahali popote isipokuwa katika makao makuu ya OFPRA iliyoko Fontenay-sous-Bois?**

Mahojiano yako yanaweza fanyika nje ya Fontenay-sous-Bois lakini kwa sababu ya umbali wako ki jiografia kwa njia ya mawasiliano ya teknolojia ya sauti na picha (haswa ukiwa ng'ambo) au kwa sababu yako ya kibinafsi (ikiwa kwa sababu ya afya au jukumu ya kifamilia, hauwezi kusafiri au ikiwa umefungiwa mahali isiyo kuruhusu kuwa huru).

Katika hali hii, ikiwa ni lazima, wakili au mwakilishi wa shirika lililo kusaidia, watakuandama. Mkalimani atakuwa pande ya afisa wa hifadhi.

Ikiwa unajipata katika eneo iliyoko nje ya nchi au katika eneo mengine ndani ya mji mkuu, unaweza hojiwa bila shaka moja kwa moja na ajenti wa OFPRA, aidha katika tawi la OFPRA iliyoko Cayenne ikiwa unaishi katika eneo la Guyana, aidha, katika eneo mengine husika, katika tukio la amri ya kazi nje ya nchi kwa msingi ya OFPRA.

## Uchunguzi ya kimatibabu.

OFPRA ina ruhusa ya kukuomba kufanya uchunguzi wa kimatibabu. Kukataa kufanya uchunguzi wa kimatibabu haitachukuliwa kama tukio la kutomaliza ombi lako na haitazuia OFPRA kuchukua maamuzi yake. Ikiwa haujahitimu umri wa mtu mkubwa na ikiwa ombi la hifadhi liliwasilishwa katika jina lako kwa sababu ya hatari ya uharibifu ya ki ngono, uchunguzi huu wa matibabu yatagharamiwa na OFPRA. Muuguzi atapeleka cheti cha matibabu moja kwa moja kwa OFPRA, na kupeana nakala moja kwa wazazi wako au msimamizi wako halali.

## Maamuzi ya OFPRA.

✓ **Muda**

Muda ya kupokea maamuzi ya OFPRA ni tofauti: Siku 15 kwa kawaida chini ya taratibu ya haraka na hadi miezi kadhaa katika taratibu ya kawaida. Kuchelewa kwa OFPRA kukupa majibu sio ishara ya kukataliwa kwa ombi lako. Ikiwa OFPRA haitaweza kufanya maamuzi kwa muda wa miezi sita, itakueleza hivyo kwa njia ya barua pepe. Unapaswa basi kuangalia barua pepe yako mara kwa mara.

✓ **Maamuzi bora** (tazama sehemu 1 « Aina mbali mbali ya hifadhi »)

Ikiwa ombi lako limefanyiwa maamuzi mazuri, utakuwa;

- **aidha utatambuliwa kama mkimbizi**, na OFPRA itakupa maamuzi ya kukutambulisha kama mkimbizi ;
- **aidha utatunukiwa haki ya hifadhi ya mbadala**, kisha OFPRA ita kufahamisha juu ya maamuzi juu ya amri ya kukuwezesha kunufaika na hali ya hifadhi mbadala pamoja na barua ya kuonyesha mbele ya serikali ili kuthibitisha hali yako ya hifadhi.

✓ **Maamuzi yasiyo bora**

OFPRA inaweza kufanya maamuzi matatu yasiyo bora kuhusu ombi lako la hifadhi:

- **Maamuzi ya kukataa ombi;**

Unaweza fanya rufaa dhidi ya maamuzi hii mbele ya CNDA. Masharti yanayo husika na haki yako ya kuwepo nchini kulingana na hali ya hifadhi zimeelezwa katika fungu la "Tamati ya haki ya kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA" katika sehemu 3.1.

- **Maamuzi ya kutoweza kupokea hati yako ya ombi** Inaweza tokea iwapo:
  - Ikiwa umeshatunukiwa hifadhi yenye ufanisi katika Mmoja wapo ya nchi za jumuia ya Ulaya;
  - Ikiwa umeshatunukiwa hali ya hifadhi na ulinzi yenye fanisi katika nchi ya tatu na ambako utarudishwa mara moja.

Unaweza pinga maamuzi hii mbele ya CNDA Hauna ruhusa ya kuendelea kuishi nchini chini ya hali ya ulinzi, hata ikiwa utafanya rufaa mbele ya CNDA (tazama "mwisho wa haki ya kuishi nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA " kakita sehemu ya 3.1).

- **maamuzi ya kutamatisha ombi lako** linaweza fanywa ikiwa:
  - ulifahamisha OFPRA kuwa ombi lako la hifadhi litupiliwe mbali wakati wa mahojiano au kwa njia ya barua ;

- ukikosa kufanya ombi lako baada ya muda wa siku 21 au hakufika katika mahojiano;
- ukifanya kusudi kukataa kupeana maelezo muhimu ya kuwezesha uchunguzi wa ombi lako;
- mawasiliano na wewe haiwezekani kwa kuwa ulikosa kupeana anwani yako ofisini kwa wakati uliyofaa.
- ombi lako liliandikishwa katika kaunta ya ki pekee lakini, bila sababu ya kutosha, haukutuma hati yako kwa OFPRA.

Unaweza pinga maamuzi hii, sio mbele ya CNDA, walakini mbele ya mahakama ya utawala. Hauna ruhusa tena ya kuendelea kukaa nchini katika hali ya hifadhi ("tazama "Tamati wa haki ya kuendelea kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA" katika sehemu ya 3.1). Kwa muda wa miezi 9 baada kuarifiwa juu ya maamuzi ya kufungwa kwa ombi lako, unaweza omba kwamba hati yako ifunguliwe upya kwa mara moja tena (tazama sehemu 3.3).

✓ **Namna ya kutumwa kwa maamuzi ya OFPRA**

**OFPRA** itakutumia maamuzi kwa maandishi ya lugha ya Kifaransa pamoja na hati iliyotafsiriwa katika lugha inayothaminika kuwa unaelewa, ilikueleza mwelekeo wa maamuzi juu yako ikiwa ombi lako lilikataliwa.

**Jee, L'OFPRA ina uwezo wa kukutumia barua ya kuthibitisha uanzilishi wa taratibu ya ombi lako la hifadhi, wito wa mkutano ya kibinafsi na maamuzi yako kwa kutumia njia isiyo husisha karatasi?**

OFPRA ilizindua mfumu inayolenga utumizi ya mawasiliano bila karatasi, kwenye akaunti ya kipekee, barua yenye kuthibitisha uanzilisha wa taratibu ya ombi la hifadhi, barua ya wito katika mkutano wa kipekee na maamuzi lililochukuliwa kuhusu ombi. Taratibu hili hufanywa katika usalama na hudhamini usiri wa ombi la hifadhi kwa ukamilifu.

Ikiwa mfumu huu itatumika kwako, utajulishwa wakati wa uandikishaji wa ombi lako la hifadhi au wakati jukumu la uchunguzi wa ombi lako la hifadhi lita amuliwa kuwa juu ya nchi ya Ufaransa ikiwa kulingana na « Dublin », lililoelezwa katika kipengele 2.2.1, ombi lako haikufuzu. Basi utapewa notisi yenye maelezo juu ya mbinu ya matumizi ya mfumo.

## ■ Kufanya rufaa dhidi ya maamuzi ya OFPRA.

Unaweza pinga maamuzi ya OFPRA mbele ya CNDA kwa muda wa mwezi moja kuanzia siku ya kupata maelezo (tazama sehemu 3.2 "Uchunguzi na CNDA). Ikiwa haukufanya rufaa mbele ya CNDA au kama ulifanya hivyo dhahiri shahiri baada ya muda iliyokubalika ya mwezi moja, haki yako ya kuendelea kukaa nchini itafika tamati, thibitisho lako la ombi la hifadhi litachukuliwa na utaamuriwa kutoka nchini Ufaransa.

Ikiwa utahitaji msaada wa kisheria kwa nia ya kufanya rufaa yako mbele ya CNDA, unapaswa kufanya ombi hili kwa muda wa siku 15 kuanzia kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA. Muda wa kufanya rufaa ambayo ni mwezi mmoja itakatizwa na itaanza kuhesabika kwa muda inayo salia kuanzia tarehe

ambayo umearifiwa kuhusu maamuzi iliyofanywa juu ya ombi lako la msaada wa kisheria (tazama fungu "msaada wa wakili" katika sehemu ya 3.2).

Maamuzi ya CNDA inaweza sababisha rufaa mbele ya Baraza la Serikali au na wewe binafsi au na OFPRA.

### ■ Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA.

Kwa msingi, una haki ya kukaa nchini kwa muda ambao ombi lako la hifadhi linachunguzwa, muda huu ikihesabu pia rufaa ya kisheria.

Hata hivyo, tamati ya haki yako ya kuendelea kukaa nchini inafika wakati utalengwa na maamuzi ya OFPRA zifuatazo:

1. maamuzi juu ya kutoweza kuandikisha ombi lako kwa sababu ulishatunukia hifadhi yenye fanisi katika nchi nyingine na, ikiwa nchi hii haiko katika jumuiya ya Ulaya, unaweza rudishwa huko (tazama sehemu ya 3.3);
2. Maamuzi ya kufunga ombi lako (tazama sehemu 3.3.);
3. maamuzi ya kukataa ombi la hifadhi chini ya taratibu ya haraka kwa sababu una uraia dhabiti;
4. maamuzi ya kukataa ombi la hifadhi chini ya taratibu ya haraka kwa sababu uwepo wako katika nchi inaweza sababisha hatari kubwa kwa hali ya umma.
5. Maamuzi ya kukataa ombi la uchunguzi upya inayobainishwa kuwa sawa;
6. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi kwa mara kwanza ya kufanya uchunguzi upya;
7. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi au kukataliwa kwa ombi wakati ambapo umelengwa na kitendo cha kufukuzwa nchini au unaweza katazwa kuishi nchini kwa sababu ya kiumma au kisheria na ikiwa ulielekezwa kwenye makazi au uliwekwa kizuizini (tazama fungu "Umelengwa na kitendo cha kufukuzwa nchini, umepigwa marufuku kuwa nchini kwa maamuzi ya serikali au mahakama? " katika sehemu 2.2.1).

Katika tukio hili, thibitisho la ombi la hifadhi linaweza chukuliwa kutoka kwako au inaweza kosa kufanya upya na amri ya kuondoka nchini lizinduliwe dhidi yako (tazama sehemu 5).

## 3.2. Uchunguzi na Mahakama ya kitaifa ya haki ya hifadhi (CNDA).

### ■ Muda wa rufaa.

Unaruhusiwa muda wa mwezi moja baada ya kuarifiwa juu ya kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA ili ufanye rufaa mbele ya CNDA. Unaweza:

- katika tukio ya kukataa kupokelewa au kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA, unaweza omba mahakama kukanusha maamuzi ya ofisi na kutunukiwa ulinzi;
- katika tukio la maamuzi inayokupa msaada wa ulinzi mbadala, unaweza omba kutambulika kama mkimbizi. Katika tukio hili, unasalia na msaada wa ulinzi mbadala, na haki zinginezo husika (tazama sehemu 6 "haki ya wapokezi wa msaada wa ulinzi"), ikiwa CNDA haitakuwa imekutunukia hali ya mkimbizi. Kwingine, ikiwa CNDA haitakutambua kama mkimbizi, haiwezi rudi kufanya maamuzi juu ya kutunukiwa kwako kwa ulinzi mbadala ambayo ulipewa na OFPRA.

Rufaa hii inafaa kufikia CNDA kabla ya kuisha kwa muda wa mwezi moja (kwa mfano, ukichukua barua ya maamuzi ya kukataliwa kwa ombi lako kutoka kwa posta tarehe 20 Januari, rufaa yako inafaa kufikia CNDA tarehe 21 Februari saa sita usiku kwa kuchelewa mno). Rufaa inapaswa kutumwa kwa CNDA kwa njia ya barua iliyosajiliwa inayo arifu juu ya upokezi wa barua, kwa barua ya kawaida au kwa kutuma nakala na barua pepe. Rufaa yako inafaa kutumwa kwa uangalifu kabla ya kuisha kwa muda iliyoruhusiwa ya mwezi mmoja au siku ya kwisha kwa muda iliyoruhusiwa kabla ya saa sita usiku ikiwa utaituma kwa njia ya barua pepe. Ikiwa mahakama itapokea rufaa yako baada ya muda inayokubalika ya mwezi moja kuisha, haitapokelewa, kumaanisha, itakataliwa bila wewe kusikizwa au kuchunguzwa.

## ■ Msaada wa wakili.

Unaweza saidiwa na wakili kwa nia ya kutayarisha rufaa na kusikilizwa kwako mbele ya CNDA. Kwa hivyo, unaweza omba kupewa msaada wa kisheria. ada ya wakili itasimamiwa kwa ukamilifu na Serikali na kwa hivyo wakali hana haki ya kukudai ada.

Ili uweze kupewa usaidizi wa kisheria, unapaswa kuwasiliana na ofisi ya msaada wa kisheria ya CNDA kwa muda wa siku 15 kuanzia siku ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA.

Anwani ya Afisi ya usaidizi ya kisheria (BAJ) ya CNDA :

Mahakama ya kitaifa ya haki ya hifadhi
35, rue Cuvier
93 558 MONTREUIL-SOUS-BOIS

Unaweza taja jina ya wakili atakaye kubali kutoa ujuzi wake kwa nia ya usaidizi wa kisheria au uulize kwamba CNDA ikukabidhi mmoja. Ikiwa utapokea usaidizi wa kisheria, hautakiwi kwa wakati wowote kulipa wakili aliyekabidhiwa, hata kama atakuuliza umlipe.

Ombi lako la usaidizi wa kisheria haitakataliwa ila ikionekana kwa kina kwamba ombi lako litakataliwa.

Wakati wa uchunguzi wa ombi lako la usaidizi wa kisheria, muda wa kufikisha rufaa yako mbele ya CNDA itakatizwa kama ombi lako liliwasilishwa katika muda inayostahili ya siku 15. Inaanza kuhesabika kuanzia siku ya kuarifiwa kwa uamuzi uliyochukuliwa na ofisi ya usaidizi wa kisheria juu ya ombi lako. Basi utatengewa wakati upya ili uweze kufikisha rufaa mbele ya CNDA, muda iliyo sawa na mwezi mmoja ukitoa siku ambazo zimepita kati ya siku ulioarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA na siku ya ombi lako la usaidizi wa kisheria.

Kwa mfano, ikiwa OFPRA ita kufahamisha maamuzi yake ya kukataa ombi lako tarehe 15 Januari, utapewa siku 15 ili kuwasilisha ombi ya msaada wa kisheria inayowezekana. Ikiwa utawasilisha ombi lako la usaidizi wa kisheria tarehe 20 Januari, yaani siku 5 baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA, utakabidhiwa siku 26 kuanzia siku ya maamuzi ya ofisi ya usaidizi ya kisheria ili kukata rufaa yako.

## ■ Kufanya rufaa.

Masharti yafuatayo ni ya kuzingatiwa:

- ya kwanza, soma kwa makini maelezo yaliyomo kwenye nyuma ya maamuzi ya kukataliwa ombi lako na OFPRA;
- rufaa inapaswa kuandikwa kwa Kifaransa kwenye karatasi nyeupe (hakuna nakala maalum) ambako utaandika jina lako la kwanza, ya pili, mahali na tarehe ya kuzaliwa, uraia wako na makao yako.

- unapaswa kutiwa sahihi kwenye rufaa yako; ukiwa mdogo wa umri, msamizi wako halali anapaswa kutia sahihi yake;
- ni lazima uambatanishe nakala ya maamuzi ya OFPRA kwa rufaa yako.
- ikiwa ombi lako la hifadhi linachunguzwa katika taratibu ya haraka, unapaswa kuambatanisha nakala ya notisi ya habari uliopewa wakati wa kuandikisha ombi lako la hifadhi (tazama fungu "kufaulu kwa hati yako ya ombi ya hifadhi" katika sehemu ya 2.2.1) ;
- unapaswa kueleza sababu yako ya kufanya rufaa, yaani kueleza sababu zako za kupinga sababu za OFPRA kukataa ombi lako au sababu zilizopelekea OFPRA kukukabidhi hali ya hifadhi mbadala badala ya kukutambua kama mkimbizi;
- unapaswa kuambatanisha hati unazo zenye kuthibitisha kitambulisho na uraia wako;
- unapaswa pia kufikisha hati zozote za kukamilisha simulizi lako;
- ukipendelea kupinga lugha iliyotumika kukuhoji katika OFPRA, unapaswa kuyasema katika rufaa yako na uashirie lugha ambayo ungependa kuhudumiwa nayo. Ikiwa mahakama itazingatia pingamizi lako na ikose kukutafutia mkalimani kwa lugha uliyo omba, utahudumiwa katika ile lugha ambayo unadhaniwa kuwa na ujuzi.
- unapaswa kuhifadhi vizuri nakala ya kutuma na kupokea rufaa yako, pamoja na nakala ya rufaa yenyewe;
- unapaswa kuarifu CNDA juu ya mabadiliko yoyote ya anwani;
- unaweza kuitisha kutumiwa hati yako baada ya kuandikishwa kwa rufaa yako.

Kwa nakala zinazo thibitisha uraia wako, imependekezwa kwamba uwasilishe nakala kwa hati na kuhifadhi nakala ya awali ya pasipoti au ya kadi yako ya kitambulisho. Umilikaji wa hati hizi inakuwezesha kupokea barua utakazo tumiwa kama barua ya kusajiliwa na CNDA kutoka kwenye posta. Unaweza wasilisha nakala za awali siku ya kusikilizwa kwa kesi yako ikiwa kamati ya hukumu itakuomba kufanya hivyo.

Kwa hati zinazo thibitisha msimulizi yako, unashauriwa kupeana nakala ya awali kwa hati ukiwa umehifadhi nakala ya picha. Unaweza tumiwa nyaraka hizi siku ya kusikilizwa kwa kesi yako, ukiomba hivyo, au zinaweza tumwa kwako baadaye kwa njia ya posta. Nyaraka za kuthibitisha msimulizi wako zinafaa kutafsiriwa kwa Kifaransa. Pasi na kutafsiriwa, CNDA haiwezi yatumia. Hata hivyo, sio lazima kwamba ukalimani ufanywe na mkalimani aliyeapishwa, isipokuwa kuhusu vitendo vya hali ya kiraia pamoja na vitendo vya sheria au vya polisi.

Unaweza, ikiwa utaitwa katika uamuzi mbele ya umma, kuwasilisha maandishi ya habari za kikamilifu hadi tarehe ya mwisho utakayo ashiriwa katika barua yako ya kukuitia mkutano.

## ■ Thibitisho la pokezi wa rufaa.

Baada ya uandikishaji wa rufaa, kwenye anuani uliyo ashiria, CNDA itakutumia hati iitwayo "thibitisho ya pokezi wa rufaa". Hati hii inaashiria kwamba rufaa yako iliandikishwa.

Isipokuwa "tazama kifungu ifuatayo juu ya "hali ya kusitisha rufaa" ), hati hii inakuwezesha kuomba kufanywa upya kwa ombi lako la hifadhi, kwa vile una ruhusa ya kuendelea kukaa nchini Ufaransa hadi siku CNDA itafanya maamuzi juu ya ombi lako.

## ■ Asili ya rufaa yenye kusababisha kusitisha maamuzi.

**Kwa namna ya jumla, una haki ya kukata rufaa mbele ya CNDA dhidi ya maamuzi ya kukataliwa ombi lako na OFPRA na rufaa hii ni ya kuahirisha mara moja** , maana kwamba unaendelea kuwa na haki ya kuendelea kukaa nchini Ufaransa hadi tamati ya muda wa rufaa na, kukiwa na rufaa, hadi wakati ambapo mahakama itafanya maamuzi yake.

**Ikiwa kwa kinyume, utapoteza haki yako ya kuendelea kuishi nchini Ufaransa kabla ya kukataliwa kamili kwa ombi lako la hifadhi** (tazama fungu "mwisho wa ruhusa ya kuishi nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA katika sehemu ya 3.1), **unahifadhi ruhusa ya kufanya rufaa mbele ya CNDA** dhidi ya maamuzi ya kukataliwa au kukataa kupokelewa kwa ombi lako na OFPRA lakini rufaa hii siyo ya kusitisha mara moja:

- ✓ **aidha rufaa siyo ya kusitisha** na maamuzi ya kurefusha ifanywe iwapo utahusika na maamuzi yafuatayo:

1. Maamuzi ya kutoweza kupokea ombi lako kwa OFPRA kwa sababu kuwa tayari umetunukiwa hifadhi yenye fanisi katika nchi nyingine na, ikiwa nchi hii sio mojawapo wa nchi za Muungano wa Ulaya, unaweza rudishwa kwenye nchi hiyo (tazama sehemu 3.3);
2. Maamuzi ya OFPRA ya kufunga kesi (tazama sehemu 3.3.);
3. maamuzi ya OFPRA ya kutoweza kupokea ombi lako la kwanza ya kuchunguzwa upya kwa kesi yako kwa sababu ya ki pekee ya kusababisha kufeli kwa juhudi za kufukuzwa nchini.

- ✓ **aidha rufaa siyo ya kusitisha mara moja na unaweza omba mahakama ya umma kusitisha utekelezaji wa kitendo cha kufukuzwa nchini iliyochukuliwa dhidi yako wakati wa kufanya rufaa yako mbele ya CNDA**, ikiwa umelengwa na mojawapo ya maamuzi ifuatayo:

  1. maamuzi ya OFPRA ya kukataa ombi lako la hifadhi chini ya taratibu ya haraka kwa madai kuwa nchi yako ya uraia imethibishwa;
  2. maamuzi ya OFPRA ya kukataa ombi chini ya taratibu ya haraka kwa madai kuwa uwepo wako nchini inachangia hatari ya hali ya umma.
  3. maamuzi ya OFPRA kukataa ombi lako la uchunguzi upya wa kesi yako hata ikiwa imethaminiwa kuwezekana;
  4. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi na OFPRA kuhusu ombi ya uchunguzi upya ambayo haikuwasilishwa ili kusababisha kufeli kwa juhudi ya kufukuzwa nchini;
  5. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi au kukataliwa kwa ombi lako wakati ambapo umelengwa na kitendo cha kufukuzwa nchini au kutoruhusiwa kuishi katika nchi kwa namna ya kiumma au kisheria na ikiwa ulielekezwa katika makao au ulitiwa kizuizini (tazama kifungu "Umelengwa na kufukuzwa nchini, kutoruhusiwa kuishi nchini kwa matamshi ya kiumma au ya mahakama?" katika sehemu ya 2.2.1).

Unaweza kuomba kusitishwa, aidha kwa hali ya kufanya rufaa dhidi ya amri ya kizuizi, aidha, ikiwa uliarifiwa juu ya amri ya kizuizi kabla ya ombi lako la hifadhi kuandikishwa na ikiwa haukuweza kufanya rufaa dhidi ya ombi hili, wakati ambapo ulielekezwa kwenye makazi ama mahali pa kizuizi, katika muda wa saa 48 baada ya kuelekezwa kwenye makazi au kutiwa kizuizini.

## ■ Usikilizaji wa kesi yako na CNDA.

CNDA itakualika katika mkutano ya usikilizaji ili kuchunguza kesi yako. Mwaliko huu itakufikia kwa njia ya barua, angalau mwezi moja kabla ya tarehe ya usikilizaji, isipokuwa kama rufaa yako itachunguzwa chini ya taratibu ya haraka na ikiwa hivyo utaalikwa kwenye mkutano siku 15 kabla ya usikilizaji.

Hata hivyo, ikiwa rufaa yako haithibitishi vipengele kubwa yenye uwezo wa kusababisha kupinga maamuzi ya OFPRA, CNDA inaweza kukataa rufaa yako kwa maagizo pekee bila kukualika katika mkutano ya usikilizaji, baada ya kuchunguza hati yako na mhariri.

Kama ni lazima, usikilizaji utafanyika:

- katika mazingira ya CNDA inayopatikana Montreuil au kwenye mahakama ya sheria (Ile de la Cité);
- aidha kwa njia ya mawasiliano ya video katika mazingira ya wizara ya haki. Usiri na dhamana bora ya uwasilishaji kupitia mawasiliano ya video yamehakikishwa.

✓ **Muundo wa hukumu:**

Muundo wa hukumu ya CNDA itakayochunguza rufaa yako inaongozwa na hakimu. Kutakuwepo pia mjuzi aliyeteuliwa na Kamati Kuu ya Umoja wa Mataifa juu ya wakimbizi (UNHCR). Muundo wa hukumu itaamuru juu ya rufaa yako baada ya kusikiliza msimulizi ambaye atachambua ombi lako la hifadhi bila kujihusisha na mwelekeo wa maamuzi, akiegemea masimulizi yako na yale ya wakili wako, ikiwa ulikuwa na mmoja.

Ikiwa afisi ilichunguza kesi yako chini ya taratibu ya haraka au ikiwa iliamua kuwa ombi lako haingeweza kupokelewa, hakimu wa ki pekee wa CNDA ndiye atatoa maamuzi kuhusu rufaa yako kwa muda wa siku tano.

Kwa juhudi zake au kwa ombi lako, mahakama inaweza amua kuchunguza kesi yako kwa muundo ya kirafiki, ikiwa itaamua kuwa ombi lako halihitaji taratibu ya haraka, sio ya kukataa kupokelewa, au ikiwa na changamoto kuu.

✓ **Ukalimani:**

CNDA huhakikisha uwepo wa mkalimani katika lugha uliyopendekeza wakati wa kuandikisha ombi lako (tazama fungu "chaguo la lugha ya mahojiano kwa OFPRA") au, badala yake au isipowezekana, lugha ambayo unaelewa vizuri. Ukipendelea kujinufaisha na kitendo cha hitilafu ya ukalimani mbele ya OFPRA, unapaswa kufanya hivyo wakati wa kufanya rufaa mbele ya CNDA. Ikiwa utasikilizwa kwa mawasiliano ya audiovisual, mkalimani atakuwa kando yako katika chumba ambako utasikilizwa. Ikiwa itakuwa vigumu kupata mkalimani awezaye kuwa kando yako kimwili, basi usikilazi hautafanyika hadi mahakama ihakikishe kwamba mkalimani mhusika awe katika chumba ambako usikilaziji utafanywa.

✓ **Uwepo wako katika usikilizaji:**

Uwepo wako katika usikilizaji unapendekezwa sana. Ikiwa utapata kizuizi au utachelewa, unaombwa kufahamisha CNDA. Ikiwa hautaweza kufika kwa usikilizaji, unaweza omba ripoti ya usikilizaji huku ukieleza kwa maandishi sababu zilizo kuzuia kufika katika usikilizaji. Ripoti hii siyo haki yako, kiongozi wa muundo wa hukumu wa CNDA ndiye atakayeamua pekee yake juu ya uwezekano wa kukutumia ripoti hii kwa tarehe ya baadaye.

✓ **Hali ya kiumma ya usikilizaji:**

Usikilizaji hufanywa mbele ya umma hata hivyo unaweza omba kiongozi wa muundo wa hukumu kwamba kesi yako isikike nyuma ya milango iliyofungwa, kumaanisha kwamba kesi yako itachunguzwa bila uwepo wa umma. Katika tukio hili, utaweza kusikika mara moja nyuma ya milango iliyofungwa. Kiongozi wa muundo wa hukumu anaweza fanya maamuzi hii pia.

## ■ Maamuzi ya CNDA.

Baada ya kuamulia kesi yako, CNDA ita kufahamisha juu ya maamuzi yake kwa njia ya posta "kwa kutumia barua iliyosajiliwa yenye thibitisho ya pokezi".

Maamuzi yanaandikwa kwa Kifaransa, ikiambatana na hati inayokuashiria mwelekeo wa maamuzi katika lugha inayoaminika kuwa una ufahamu.

Katika maamuzi, CNDA inaweza:

- kanusha maamuzi ya kukataa kwa mbi lako na OFPRA na kukutunukia hali ya mkimbizi au kukupa msaada wa ulinzi mbadala. Basi utaweza kufaidika na haki sawa na ikiwa ungetunukiwa moja ya aina hizi za ulinzi na OFPRA ;
- Kukanusha maamuzi ya OFPRA ya kukutunukia ulinzi mbadala na kukutunukia hali ya mkimbizi;
- thibitisha maamuzi ya OFPRA ya kukataa ombi lako na kukataa rufaa yako;
- wakati mwingine, kukanusha maamuzi ya OFPRA na kuiomba kuchunguza ombi lako upya.

Maamuzi ya CNDA inaweza lengwa na rufaa mbele ya mahakama kuu au Baraza la Serikali. kamati hii haichunguzi ombi lako kwa jumla, ila tu vipengele vinavyo gusia maswala ya kisheria. Taratibu hii ni ya muda mrefu na inahitaji wakili mtaalamu. Unaweza omba msaada wa kisheria. Rufaa hii haitaruhusu kurefusha muda wako wa kukaa nchini Ufaransa na haitazuia urudishwe kwenye nchi yako ya uraia. Imependekezwa kuwa upate habari kamili juu ya taratibu hii kutoka kwa shirika husika au wakili.

### ■ Tamati ya ruhusa ya kuendelea kukaa nchini kufuatia maamuzi ya CNDA.

Ruhusa yako ya kukaa nchini inafika tamati iwapo:

-wakati wa kusomwa kwa maamuzi ya CNDA ikiwa itaamuru katika usikilizaji wa umma. Utaarifiwa juu ya maamuzi kwa kila sababu ya chanzo ;

- wakati wa kuarifiwa juu ya maamuzi ya CNDA ikiwa itafanywa kwa maagizo.

Punde ruhusa yako ya kukaa nchini itafika tamati, ni lazima uondoke nchini Ufaransa na unaweza lengwa na amri ya lazima ya kuondoka nchini Ufaransa "tazama sehemu 5).

## 3.3. Kufunguliwa upya kwa ombi la hifadhi lililofungwa.

katika tukio la kufungwa kwa uchunguzi wa ombi lako (tazama fungu "maamuzi ya OFPRA" katika sehemu 3.1), kwa mara moja tu, unaweza fanya ombi la kufunguliwa upya kwa muda wa miezi 9 baada ya uamuzi wa kufunga kesi. Kwa hivyo, unapaswa kufika kwenye idara ya pokezi wa kwanza wa waomba hifadhi (SPADA) kisha katika kaunta ya ki pekee ili kujiandikisha upya (tazama sehemu 2).

Kisha umepewa hadi siku 8 baada ya uandikishaji wa kesi yako ili kuwasilisha ombi lako la kufunguliwa upwa kwa kesi mbele ya OFPRA, ambayo itazindua hati yako upya na itaendelea na uchunguzi wa ombi lako la hifadhi kuanzia mahali ambapo ilisimamishwa.

Katika tukio la ombi la kufunguliwa upya kwa muda wa miezi 9, unanufaika upya na haki ya kuendelea kukaa nchini na utatumiwa thibitisho ya ombi la hifadhi.

Miezi 9 ikipita, ombi lako la kufunguliwa upya kwa kesi yako itachukuliwa kama ombi la uchunguzi upya (tazama 3.4 "Uchunguzi upya ").

## 3.4. Uchunguzi upya.

Baada ya kukataliwa kwa ombi lako la hifadhi na CNDA au ikiwa haukufanya rufaa kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA, una uwezo wa kuomba OFPRA kuchunguza ombi lako upya kwa masharti kwamba "vipengele vipya" vijitokeze, maana yake:

- vipengele ambazo zimejitokeza baada ya tarehe ya maamuzi ya CNDA au kabla ya maamuzi lakini ambazo ulifahamu baadaye;
- vipengele zenye kuthibitisha hofu yako ya mateso au hatari ya vitisho kuu zinazoweza fanywa juu yako ukirudi kwenye nchi yako.

Unaweza tafuta mawaidha kwa shirika husika au wakili.

Ikiwa unawasilisha ombi la uchunguzi upya wa kesi yako, unapaswa kujiwasilisha mbele ya idara ya mapokezi ya kwanza ya wakimbizi (SPADA) kisha kwenye kaunta ya ki pekee ili ujiandikishe upya (tazama sehemu 2).

Una hadi siku 8 kuanzia siku ya uandikishaji upya wa ombi lako ili kuwasilisha ombi lako la uchunguzi upya mbele ya OFPRA. Ikiwa ombi lako haitakuwa na hati kamili, ofisi itakuomba kuikamilisha kwa muda wa siku 4.

Kisha OFPRA itaanza uchunguzi wa awali wa ombi lako na kufanya maamuzi juu ya kukubalika kwa ombi lako kwa muda wa siku 8 baada ya kuipokea. Wakati wa uchunguzi huu, sio lazima uitiwe mkutano wa mahojiano.

Baada ya uchunguzi huu, OFPRA itaweza kuamuru kuwa ombi lako la uchunguzi upya haikubaliki ikiwa habari au vipengele unaopeana hayata boresha uwezekano wako wa kutunukiwa ulinzi wowote.

Ikiwa OFPRA itaamua kukubali ombi lako, litachunguzwa kwa dhati na kushughulikiwa, isipokuwa kuwepo na maamuzi ya kinyume, katika taratibu ya haraka.

Tukio la maamuzi ya kutokubalika au ya kukataliwa kwa ombi lako la uchunguzi upya na OFPRA inaweza sababisha rufaa mbele ya CNDA (tazama sehemu 3.2).

**Jee, unaweza faidika na haki ya kuendelea kukaa nchini kwa muda ambao ombi lako la kuchunguzwa upya kwa kesi yako ikifanyika?**

Katika tukio la ombi la kwanza la uchunguzi upya (tazama fungu "Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini baada ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA" katika sehemu 3.1) :

- Ikiwa ofisi ya wilaya itabaini kuwa ombi lako lilifanywa kwa nia ya ki pekee ya kufeli kwa juhudi za kufukuzwa nchini, na kuwa OFPRA ilikataa kupokea ombi lako, hutaruhusiwa tena kukaa nchini kuanzia siku ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA na kitendo cha kufukuzwa nchini inaweza amuliwa juu yako na ichukuliwe hatua.

- kama OFPRA ilipendelea kutokubali ombi lako lakini ofisi ya wilaya inabaini kuwa ombi hili halikufanywa kwa nia ya ki pekee ya kufanya kufeli kwa juhudi ya kufukuzwa nchini, hutaruhusiwa kuendelea kukaa nchini mara tu utakapo arifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA na amri ya kizuizi inaweza

fanywa dhidi yako lakini unaweza omba kusitishwa kwa amri hii ili isichukuliwe hatua mbele ya mahakama ya umma wakati ukisubiri kukata rufaa mbele ya CNDA ;

- Ikiwa OFPRA iliamuru kuwa ombi lako linakubalika na baadaye kukanusha maamuzi haya, hutaruhusiwa tena kuendelea kukaa nchini kuanzia siku ya kuarifiwa juu ya maamuzi ya OFPRA na amri ya kizuizi inaweza fanywa juu yako lakini unaweza omba kusitisha ichukuliwa hatua mbele ya mahakama ya umma ukisubiri kukata rufaa mbele ya CNDA.

Katika tukio la ombi la pili la uchunguzi upya wa ombi lako, haunufaiki na ruhusa hii ya kuendelea kuishi nchini. Juhudi ya kufukuzwa nchini inaweza fanywa juu yako na kuchukuliwa hatua, na ifanyike bila kusubiri maamuzi ya OFPRA.

# 4. Vifaa vya mapokezi ya muomba hifadhi na haki yake

Kama muomba hifadhi, una haki ya kunufaika na vifaa  vya mapokezi ambazo ni:

- makazi katika kituo cha kupokea waomba hifadhi (CADA) au kituo cha makazi ya dharura, kwako na kama ni lazima, familia yako (sehemu 4.1) ;
- Msaada wa kifedha ya kila mwezi ya muomba hifadhi (ADA), ambapo kiwango italinganishwa na muundo wa familia yako (sehemu 4. 2).

Wakati wa mkutano wako katika kaunta ya ki pekee ili kuandikisha ombi lako la hifadhi, OFII itakufanyia pendekezo la kugharamiwa inayo thibitisha vifaa vyako vya pokezi (tazama sehemu 2.2.2).

Utanufaika vile vile na uongozi katika shughuli zako za kiutawala na za kijamii ili kuhakikisha kufuatilia hati yako ya ombi la hifadhi na kunufaika na haki za kijamii uliopewa, haswa kuhusu elimu, afya na kazi (sehemu 4. 3 hadi 4. 5).

## 4.1. Kupewa malazi kwa muomba hifadhi.

### ■ Mahali pa malazi

Mahali ya malazi ni vituo vya pokezi vya waomba hifadhi (CADA) na makazi ya dharura ya waomba hifadhi kwa jumla (HUDA) Maeneo ya malazi yanagharamiwa na utaratibu yanafanywa na serikali.  Kwa mara nyingi, eneo hizi za malazi yana simamiwa na mashirika.

Kuna tarakimu makao 100,000 zilizotengewa waomba hifadhi na zimetawanyika katika ujumla wa taifa la Kifaransa, kwa njia ya  jengo la ghorofa, vituo vya kijamii au vyumba vya hoteli. Katika CADA na katika HUDA, kuna uwezekano wa utumizi wa kijamii ya sehemu zingine za nyumba kama (jikoni, bafu na choo) pamoja na wakazi au familia zingine.

Ili unufaike na makazi, unafaa kutunukiwa thibitisho la ombi la hifadhi yenye fanisi.

Kuhusu CADA na HUDA, utanufaika na mwongozo katika shughuli za kiutawala na kisheria (katika taratibu ya hifadhi na uongozi wa kiusafi na kijamii (uandikishaji wa haki za kijamii, kupewa matibabu, elimu ya watoto na kadhalika.)  Ikiwa unakaa katika chumba cha hoteli, unaweza nufaika na uongozi haya kutoka kwa kifaa cha makaribisho ya kwanza kwa waomba hifadhi (SPADA).

### ■ Maelekezo kwenye makazi.

OFII iliyoko katika kaunta ya ki pekee (GUDA) ambako uliandikisha ombi lako la hifadhi  ita kupendekezea vifaa vya makaribisho au (CMA), ambayo inahusu pia makazi na msaada wa kifedha ya muomba hifadhi (ADA):

- **ukikataa pendekezo hili la kugharamiwa** , hutapendekezewa manufaa ya CMA.
- **ukikubali pendekezo la kugharamiwa** ,kulingana na aina ya taratibu la ombi lako la hifadhi na uwepo katika eneo, kanda au nchini Ufaransa kwa jumla, OFII ita kupendekezea mahali katika CADA au malazi ya dharura (HUDA).

Unaweza pendekezewa makazi nje ya eneo au kanda ambako uliandikisha ombi lako la hifadhi. Ukikataa pendekezo hili, hautaweza kamwe kupokea ADA na hautafanyiwa pendekezo lolote la makazi.

Katika tukio la ukosefu wa makazi, OFII itakuelekeza kwenye SPADA ambako watakutafutia makazi.

### ■ Kuingia na kuondoka kwenye makazi.

**Ikiwa umekubaliwa kuingia katika CADA au HUDA**, unaruhusiwa kuishi huko kwa muda wote wa kuchunguzwa kwa ombi lako la hifadhi (OFPRA na CNDA).

Hata hivyo, katika tukio zingine, muda wako wa kuishi itakatizwa kutokana na maamuzi ya OFPRA kukataa ombi lako (tazama kifungu "Msaada wako wa vifaa vya makaribisho yanakatishwa wakati upi?" katika sehemu 4. 2.).

**Ukitunukiwa hali ya ukimbizi au manufaa ya ulinzi mbadala**(maamuzi bora kamilifu ya OFPRA au ya CNDA), unapaswa kuondoka kwenye CADA au HUDA baada ya muda wa miezi tatu, na uwezekano wa kurudiliwa mara moja.  Ikiwa utaendelea kuishi katika makao kupita muda huu, unaweza fanyiwa taratibu ya kufukuzwa mbele ya hakimu wa sheria.

Ikiwa ombi lako la hifadhi limetupiliwa mbali (maamuzi mbaya kamilifu ya OFPRA au CNDA), unapaswa vile vile  kuondoka katika CADA au HUDA mnamo kuisha kwa haki yako ya kuendelea kukaa nchini (tazama kifungu "tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini" katika sehemu 3.1 na 3.3), isipokuwa chini ya hali spesheli  iliyotengwa na sheria.

**Ukiendelea kukaa kwenye makao baada ya muda uliotengwa**, unaweza fanyiwa taratibu ya kufukuzwa nchini.  Katika hali hii, uta arifiwa kutoka kwenye makao na mkuu wa wilaya, au meneja wa CADA au wa HUDA. Ikiwa hautafanya hivyo, mkuu wa wilaya au meneja ataweza kuwasiliana na hakimu wa utawala ili akuamuru kutoka kwenye makao.  Ikitakikana, afisa wa polisi ya kimataifa au afisa wa mgambo wa kitaifa watatekeleza kufukuzwa kwako kutoka kwa makao.

## 4.2. Msaada wa muomba hifadhi (ADA).

Usimamizi wa msaada wa muomba hifadhi (ADA) unatekelezwa na OFII na malipo kufanywa na shirika la huduma na malipo.

Utapewa msaada huu kwa njia ya kadi itakayopewa na OFII, ikiwa kama muomba hifadhi, una haki ya kuendelea kukaa nchini au hadi upitishwe kwa ufanisi katika nchi nyingine iliyoko na jukumu ya kuchunguza ombi lako la hifadhi.

### ■ Masharti ya kunufaika na msaada huu.

Ili unufaike na msaada wa muomba hifadhi, unafaa:

1-kumiliki thibitisho la ombi la hifadhi;

2- uwe na umri wa miaka 18;

3- ukiwa muomba hifadhi, uwe umekubali vifaa vya makaribisho ya kupendekezwa na OFII wakati wa mkutano wako nao katika kaunta ya ki pekee.

**Jee, naweza nufaika na vifaa vya makaribisho bila kumiliki thibitisho ya ombi la hifadhi?**

Kama ilivyo ashiriwa awali, unapaswa kumiliki thibitisho la ombi la hifadhi yenye ufanisi ili kunufaika na viyaa vya makaribisho.

Kata hivyo, unaweza kosa kunufaika na vifaa vya makaribisho ikiwa uliwasilisha omba kuchunguzwa upya kwa ombi lako au uliomba hifadhi kuchelewa sana, bila sababu halali (tazama kifungu «kufuzu kwa ombi lako la hifadhi" katika sehemu 2.2.1), hata ikiwa unamiliki thibitisho ya ombi la hifadhi.

Kwingine, waomba hifadhi ambao thibitisho lao la ombi la hifadhi ilikataliwa au haikufanywa upya kufuatia maamuzi ya OFPRA kukataa ombi lako la hifadhi iliyofanywa katika harakati ya haraka kwa maudhui mengine (nchi yako ya uraia imethibitishwa, hatari kubwa kwa hali ya umma),wataendelea kunufaika na msaada wa vifaa vya makaribisho baada ya maamuzi ya OFPRA, na kufuatia rufaa mbele ya CNDA, hadi wakati ambapo hakimu ataamulia kesi yake (hakimu wa utawala au hakimu wa hifadhi). Ni muhimu kukumbuka kwamba, katika hali hii, msaada wa kifedha inaweza badilishwa na msaada wa vifaa.

## Muundo wa ombi.

Ukiwa muomba hifadhi, haki ya msaada wa kifedha ya muomba hifadhi inafunguliwa baada ya kuandikisha ombi lako la hifadhi kwenye kaunta ya ki pekee kwa masharti kwamba ukubali mapendekezo ya kugharamiwa utakaopewa na OFII.

Malipo ya msaada huu utaanza baada ya kuwasilisha hati yako ya ombi la hifadhi kwenye OFPRA kwa muda wa siku 21 kwa kuchelewa sana baada ya kuandikisha ombi lako la hifadhi.

## Kiwango cha msaada.

Ili unufaike na msaada wa kifedha ya muomba hifadhi, unafaa kuthibitisha kuwa rasilimali zako za kifedha ziko chini ya mapato ya mshikamano inayotumika (RSA).

Kiwango cha msaada wa kifedha unahesabiwa kulingana na kiwango inayotilia maanani muundo wa familia yako, mapato yako na aina ya makao yako.

## Malipo.

Malipo ya kwanza ya msaada kwa muomba hifadhi itafanyika baada ya kuwasilisha hati yako ya ombi la hifadhi kwa OFPRA. Ikiwa ulipeana nambari ya simu ya rununu kwa OFII, utatumiwa ujumbe wa kukuarifu kwamba kadi yako imejazwa na malipo.

Malipo itafanywa hadi mwisho wa mwezi ambayo haki yako ya kuendelea kukaa nchini itafika tamati (tazama fungu "Tamati ya haki ya kuendelea kukaa nchini" katika sehemu 3.1 na 3.2).

Malipo ya kifedha itakatizwa mwisho wa mwezi inayofuata mwezi uliyoarifiwa kuhusu maamuzi kamili inayohusiana na ombi lako la hifadhi.

### ■ Kufanya rufaa.

Unatakiwa kwa kina kuarifu OFII juu ya mabadiliko yoyote kuhusu hali yako, iwe ni kuhusu kuishi kwako nchini, muundo wako wa kifamilia, ya rasilmali yako au ya ajira yako.

Ikiwa utakata rufaa dhidi ya maamuzi ya ADA iliyochukuliwa na OFII, ni jukumu lako kukata rufaa ya ukaguzi mbele ya OFII, mahakama ya kiutawala nayo inawajibika na rufaa ya mashaka.

**Msaada wako wa kifedha wa makaribisho yatatiwa tamati wakati upi?**

Manufaa ya msaada wa kifedha ya makaribisho yatafika tamati mwisho wa mwezi ambayo haki yako ya kuishi nchini ilifika tamati katika hali ya hifadhi.

Waomba hifadhi ambao haki yao ya kuishi nchini imefika tamati kufuatia maamuzi ya kukataliwa kwa ombi lao na OFPRA chini ya ombi iliyowekwa kwenye taratibu ya haraka kwa sababu zingine kama (nchi ya uraia thabiti, hatari kubwa kwa hali ya umma) watanufaika na msaada wa kifedha hadi mahakama ikatae ombi la kusimamishwa kwa utekelezaji wa juhudi ya kufukuzwa nchini ama hadi CNDA ifanye maamuzi yake (tazama sehemu 5.1).

Ikiwa utatunukiwa hali ya mkimbizi au unufaishwe na ulinzi mbadala, manufaa ya msaada wa kifedha itafika tamati kwa mwezi ifuatayo mwezi ambayo uliarifiwa juu ya maamuzi haya.

Hata hivyo, msaada wa kifedha unaweza simamishwa ikiwa:

-bila sababu halali, umetoroka kutoka kwa mahali pa malazi;

-haukutii wajibu wa kukusalimisha mbele ya serikali, hakupeana majibu kuhusu ombi la habari au haukufika katika mahali pa mahojiano ya kibinafsi kuhusu taratibu ya hifadhi;

-OFII ilikuelekeza kwenye eneo ya malazi au SPADA katika eneo tofauti lakini ukakosa kufika huko katika muda wa siku 15 tarajiwa;

-OFII ilikueleza kwenye eneo nyingine na ukatoka huko bila kuruhusiwa na OFII.

-ulificha ukweli kuhusu rasilimali yako ya kifedha;

-ulisimulia habari ya uongo kuhusu hali yako ya kifamilia;

-uliwasilisha ombi kadhaa ya hifadhi chini ya vitambulisho tofauti ;

-ulifanya mvurugano mkuu au kwa njia kubwa haukutilia maanani sheria ya kituo chako cha makazi.

Maamuzi yatafanywa baada ya kuwezeshwa kuandikisha maoni yako mbele ya OFII. Ikiwa ulificha ukweli kuhusu rasilmali yako ya kifedha, ulisimulia habari ya uongo kuhusu hali yako ya kifamilia na kuwasilisha ombi nyingi ya hifadhi chini ya vitambulisho tofauti, tukio hizi zinaweza sababisha uombwe kurudisha fedha ambazo ilipewa kinyume na masharti.

## 4.3. Fursa ya kupata elimu

Fursa ya kuingia katika mfumo wa elimu kwa watoto wa waomba hifadhi ni sawa ni ile iliyotengewa wananchi.

Kulingana na kanuni ya elimu (makala L.111-2), "*watoto wote wana haki ya masomo ya shule ambayo, kwa nia ya kukamilisha matendo ya familia, inachangia elimu yake* ». Kumbuka kwamba « *elimu ni lazima kwa watoto wa jinsia zote mbili, Wafaransa au wa nje, wa miaka 6 na 16* »(makala L.131-1 ya kodi ya iliyotajwa awali).

Usajili kwa shule ya msingi inafanyika kwa ofisi ya meya. Unafaa kuwasilisha hati ya kuthibitisha uhusiano wako na mtoto, makazi yako na kwamba mtoto amefanyiwa chanjo kwa sasa.

Usajili katika kituo cha elimu ya shule ya sekondari (chuo cha elimu au chuo cha upili) inafanywa moja kwa moja katika kituo cha elimu iliyoko karibu na eneo lako la makazi.

Idara inayo jukumu ya kukuongoza katika maswala ya kitawala inaweza kukupa msaada ili ukamilishe shughuli za kisheria au ya kijamii, za kuhusu idara inayo shughulika na makazi yako au idara ya makaribisho ya kwanza (SPADA) chini ya mwito wa OFII (tazama nukta 2.1)

## 4.4. Fursa ya kupata matibabu

### ■ Jee, unaweza pata matibabu wapi?

- **Kwa mtaalam wa afya (nje ya hospitali)**

Kwa tatizo zote za kiafya, unaweza shauriana na daktari "wa jumla" ambaye atakuchunguza na kukuandikia madawa ambazo unahitaji. Atakuelekeza kwa daktari "mtaalam" au kwa daktari msaidizi (muuguzi, muuguzi wa viungo vya mwili...) ukiwa na mahitaji ya uchunguzi au tiba ya ziada.

- **Katika duka ya dawa:** ili kununua dawa ama kutafuta mawaidha.

- **Katika hospitali:** kwa hali ya dharura, au kwa kufanya miadi ya kufanya uchunguzi zingine au kushauriana na mtaalam.

**Matibabu haya ni ya kulipwa ingawaje zinaweza gharamiwa na bima yako ya matibabu** (tazama aya ifuatayo).

**Ukiwa unasubiri kupata bima yako ya matibabu, unaweza tibiwa bila malipo katika idara zifuatazo** :

- Kwa aina zote za matibabu:
    - unaweza enda kwenye vituo vinavyo ajibika na kupeana matibabu ya kiafya (PASS) kwa kawaida zinapatikana katika vyumba vya hospitali. Utahudumiwa bila malipo na daktari na utapewa madawa bila malipo.
    - shirika mengine yenye taaluma (Médecins de Monde , le COMEDE...) hupendekeza ushauriano na daktari wa jumla bila malipo, ushauriano na daktari wa meno, au ushauriano ya kitaalamu (magonjwa ya uzazi, magonjwa ya macho au kisaikolojia na kadhalika.)
- Kwa shida maalum ya kiafya
    - Kwa uchunguzi wa mama wajaa wazito, uchunguzi na chanjo ya watoto walioko chini ya miaka 6:kwenye kituo cha PMI (Ulinzi ya uzazi kwa watoto)
    - Kwa uchunguzi wa kifua kikuu: kwenye CLAT (kituo cha kupambana dhidi ya kifua kikuu)

- Kwa uchunguzi wa UKIMWI, homa manjano au magonjwa ya zinaa: katika Vituo vya habari bila malipo, ya uchunguzi na utambuzi (CeGIDD)
- Kwa pokezi wa vifaa vya kupanga uzazi: katika kituo cha upanga uzazi (CPEF)
- Kwa utegemezi ya madawa ya kulevya: kwenye kituo cha matibabu, uongozi na kinga ya utegemezi (CSAPA)

**Tafuta maelezo zaidi kwenye idara ya makaribisho ya kwanza ulioko, mahali pako pa malazi au hospitali ya karibu ili kujua mahali pa kuzipata au tazama** http ://annuairesante.ameli.fr

**Kwa mahitaji ya matibabu ya dharura** , piga simu kwa nambari 15 au 112, au uende kwenye kituo cha tiba ya dharura ya hospitali iliyoko karibu nawe ikiwa hauwezi kupiga simu.

## Jee, unawezaje pata msaada ya gharama ya karo ya matibabu yako

**Nchini Ufaransa, matibabu ni ya malipo lakini unaweza nufaika na bima ya afya iwezayo kugharamia malipo yako ya tiba aidha kwa kikamilifu au kwa upande.**

Inahusu ulinzi wa jumla wa afya (PUMa) vile vile msaada wa ziada ya afya ya kijamii (CSS). Msaada lililotajwa mwisho hutolewa kulingana na hali ya uwezo wa kifedha.

Mifumo hii inagharamia matibabu yako yote ya kawaida, ikiwemo pia miwani, viziba meno na kadhalika. La ziada, msaada wa ziada ya afya ya kijamii itakuwezesha kupata tiba haya bila malipo, na pia kipunguzo kwa nauli yako.

**Unaweza omba kunufaika nayo kwenye shirika ya bima ya kikanda (CPAM) ilioko katika eneo unakoishi:**

- **mara tu baada ya usajili wa ombi la hifadhi ya watoto wako:**unapaswa kujaza fomu ya "Ombi la kufunguliwa kwa haki ya kupewa bima ya afya" na ya " Ombi la msaada wa ziada ya afya ya kijamii" na kujumuisha thibitisho la ombi la hifadhi inayohusika ;

- **baada ya kuishi ufaransa kwa muda wa miezi tatu, wewe (au mchumba wako):** unapaswa kujaza upya fomu hizi na zaidi ya thibitisho lako la ombi la hifadhi, unapaswa kuwasilisha vile vile thibitisho kwamba umeishi nchini ufaransa kwa muda iliyo juu ya miezi tatu, kwa mfano: thibitisho ya makazi iliyotolewa na kituo cha malazi kwa miezi tatu zilizopita; thibitisho ya makazi iliyo na tarehe ya kuzidi miezi tatu; thibitisho ya ombi la hifadhi yenye tarehe ya kuzidi miezi tatu; hati zote zilizotolewa na shirika ya mapokezi ya dharura kwa waomba hifadhi (SPADA) iliyo na tarehe ya kuzidi miezi tatu; ikiwa umepewa makazi na mhusika wa tatu, basi thibitisho juu ya heshima ya mtu huyu itakayo onyesha mwanzo wa makazi vile vile ushahidi ya makazi (malipo ya kodi, malipo ya stima.....) iliyoandikwa kwa jina yake, kwa muda wa miaka tatu zilizopita na kadhalika.

Ikiwa wewe au mtoto wako mnahitaji tiba ya dharura, unaweza ambatisha ushahidi ya hitaji ya tiba ya dharura, ili kuharakisha uchunguzi wa kesi yako na unufaike na bima yako ya afya haraka iwezekanavyo.

Katika harakati hii, unaweza pata msaada kutoka kwa shirika ya mapokezi ya dharura kwa waomba hifadhi (SPADA), kituo chako cha malazi (CADA, HUDA…) ama vile vile katika idara ya huduma za kijamii ya hospitali.

**Bima yako ya afya itafunguliwa kwa matumizi tarehe ambayo utawasilisha kesi yako kwa CPAM. Basi ni muhimu ufanyi ombi lako bila kusubiri ya watoto wako (mara tu utaandikisha ombi lako la hifadhi), na mara tu utaweza kutoa ushahidi ya kukaa nchini ufaransa kwa zaidi ya miezi tatu, kwako ama kwa mchumba wako.**

utapokea thibitisho utakayopea muuguzi, hospitalini au kwenye duka la dawa ili upate tiba. Itatumwa kwako na hazina katika anuani iliyo kwenye fomu: unapaswa kuandika anuani ya mahali pako pa makazi katika fomu hiyo. l

Utanufaika na bima ya afya kwa wakati wa utaratibu , kisha baadaye ikiwa utatunukiwa msaada wa ulinzi wa kimataifa. Kwa vile msaada wa ziada ya afya ya kijamii inadumu kwa muda wa mwaka mmoja tu, unapaswa kuwasilisha kesi mpya kila mwaka ili uendelee kunufaika nayo, imependekezwa iwe angalau miezi 4 au 2 kabla ya tamati ya haki ya kuitimia, ilivyo andikwa kwenye thibitisho lako.

**Ukisubiri kufunguliwa kwa haki yako ya matumizi, unaweza pata matibabu bila malipo kwa tiba ya kawaida katika vifaa zisizo lipisha zilizotajwa katika sehemu ya awali "unaweza pata wapi tiba?".**

**Tiba zako "za muhimu" zitagharamiwa pia katika hospitali.** Hizi tiba ni zile zisizoweza subiri, kwa mfano: tiba ya jeraha ya kina, mvunjiko, kuchomeka, ugonjwa hatari au ya kuambukiza, tiba yote ya watoto wachanga au wamama wajawazito(haswa ukaguzi kwa sababu ya kinga inayofanywa kwenye na baada ya mimba, kuzaa, kuavya mimba...)**unapaswa kuonyesha thibitisho lako la ombi la hifadhi wakati utakuja hospitalini ili upate tiba bila malipo.**

**KUMBUKA :**

**Utawasilisha ombi la bima ya afya kwenye CPAM iliyoko eneo lako la makao mara utakaposajili ombi lako la hifadhi kwa watoto wako wachanga, na pia wewe mwenyewe (au mchumba wako) mara utakapo fikisha zaidi ya miezi tatu nchini Ufaransa.**

**Ukisubiri kunufaika na bima ya afya, unaweza pata tiba bila malipo katika vifaa mbali mbali vya matibabu ama ili upate tiba ya "maradhi ya haraka" katika hospitali: utaonyesha thibitisho lako la ombi la hifadhi.**

**Unapaswa kufahamisha CPAM ya eneo lako kila hali yako itakapo badilika:**utatuma nakala la thibitisho kila ombi lako la hifadhi litakapo rudiliwa, thibitisho mpya ya makazi, na nakala ya risiti ya ombi la kibali cha kuishi ikiwa utanufaika na ulinzi wa kimataifa.

## 4.5. Ushiriki katika soko la ajira.

Kama muomba hifadhi, unaweza ruhusiwa kufanya kazi ikiwa OFPRA, kwa sababu zisizo wajibika, haikufanya maamuzi juu ya ombi lako la hifadhi katika muda wa miezi sita kuanzia kupokelewa kwa ombi lako.

Katika tukio hili, kwa kuonyesha ombi la ruhusa ya kufanya kazi iliyoandikwa na mwajiri wako, unaweza fanya ombi la ruhusa ya kufanya kazi kutoka kwa huduma ya kazi (SMOE) ya DIRECCTE iliyoko kwenye idara yako ya makao.

Maamuzi kuhusu ombi la ruhusa ya kufanya kazi inachukuliwa na mkuu wa wilaya/DIRECCTE/SMOE, ombi lina chunguzwa kwa muda wa miezi mbili kuanzia siku ya kuandikisha ombi. Usipo pokea jibu

kwa muda huu, itachukuliwa kama ombi imekubaliwa. Itaarifiwa kwa mwajiri wako wa usoni pamoja na wewe mwenyewe, na inatumika kwa wakati ambapo utaruhusiwa kuishi nchini.

Ikiwa utapewa ruhusa ya kufanya kazi, mkuu wa wilaya atatuma ruhusa ya kazi ikizingatia kandarasi ya muda iliyozidi miezi 3 au kwa kandarasi ya kazi ya misimu kwa OFII.

Hata hivyo, unaweza nyimwa ruhusa hii, sana sana kwa kutilia maanani hali ya ajira katika eneo lako au sekta husika, isipokuwa kama utatafuta kazi iliyo tambulika katika orodha ya taaluma zilizo na ugumu ya kupata wafanyikazi.

Ikiwa ulitunukiwa ruhusa ya kufanya kazi kwa muda mfupi na katika tukio la mkataba wako kufikia tamati kwa sababu zisizo za hiari yako au ikiwa mkataba wako wa muda inayojulikana au mkataba wa muda mfupi utafika tamati, unaweza omba kusajiliwa kama mtafuta ajira katika kituo cha Pôle emploi.

Ukiwa mtoto mdogo ambaye hafuatwi na mtu mzima na unanufaika na ruhusa ya kufanya kazi ili kukamilisha kandarasi ya somo au taaluma kwa muda unaojulikana, unaweza fuatilia kandarasi yako ukiwasilisha ombi la hifadhi kuanzia tarehe 1 mechi 2019.

Mwishowe, ukiingia katika soko la ajira, utanufaika vile vile na masharti yaliyo tolewa na kodi ya kazi, ya utendaji wa masomo ya kitaalam.

# 5. matokeo ya kukataliwa kwa ombi lako la hifadhi kuhusu haki yako ya kuendelea kukaa nchini

## 5.1. Maamuzi ya kukataliwa kwa ombi lako na OFPRA au CNDA

### ■ Tamati ya haki ya kukaa nchini baada ya kuarifiwa kwa maamuzi ya OFPRA.

✓ **Rufaa mbele ya CNDA haisitishi:**

Kama ilivyo andikwa katika sehemu ya 3.1, haki yako ya kuendelea kukaa nchini itafika tamati iwapo umelengwa na mojawapo ya maamuzi ya OFPRA yafuatayo:

1. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi lako kwa sababu kwamba umeshatunukiwa ulinzi iliyo halali katika nchi nyingine, ikiwa nchi hii haiko katika jumuiya ya Uropa, unaweza rudishwa huko (tazama sehemu 3.3);
2. maamuzi ya kufunga kesi (tazama sehemu 3.3.);
3. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi lako kwa mara ya kwanza ya kuomba uchunguzi upya iliyofanywa ikiwa umelengwa na juhudi ya kufukuzwa nchini.

katika hali hii, unaweza nyang'anywa thibitisho la ombi la hifadhi au ikose kurudiliwa na upewe amri ya lazima ya kutoka nchini Ufaransa. Kufanya rufaa mbele ya CNDA haisababishi kusitisha kesi yako na amri ya kufukuzwa nchini inaweza chukuliwa hatua dhidi yako kwa wakati wowote.

Ikiwa ulijulisha OFPRA kuwa ombi lako la hifadhi litupiliwe mbali, utapoteza haki ya kuendelea kukaa nchini na rufaa mbele ya CNDA haitaweza sitisha maamuzi huu.

✓ **Rufaa mbele ya CNDA sio ya kusitisha maamuzi kwa mara moja:**

Haki yako ya kuendelea kukaa nchini itafika tamati pia ikiwa umelengwa na mojawapo ya maamuzi ya OFPRA ifuatayo:

1. maamuzi ya kutoweza kupokelewa kwa ombi lenye kufanywa upya kwa mara ya kwanza ikiwa ombi hili lilifanywa bila wewe kulengwa na juhudi ya kufukuzwa nchini;
2. maamuzi ya kukataliwa kwa ombi la uchunguzi upya ikiwa ombi haijakubalika;
3. maamuzi ya kukataa ombi la hifadhi iliyowekwa chini ya taratibu ya haraka kwa madai kuwa nchi yako ya uraia imethibitiwa;
4. maamuzi ya kukataa ombi la hifadhi iliyowekwa chini ya taratibu ya haraka kwa madai kwamba uwepo wako katika nchi unachangia hatari kuu kwa hali ya umma
5. maamuzi ya kutoweza kupokea ombi au kulikataa ikiwa ulilengwa na kitendo cha kufukuzwa nchini au kukatazwa kuishi nchini kwa njia ya kiutawala au kisheria na ikiwa ulipewa makazi au uliwekwa kizuizini (tazama fungu "umelengwa na kitendo cha kufukuzwa nchini, kukatazwa kuishi nchini iliyofanywa na utawala au na mahakama?" katika sehemu ya 2.2.1).

Kwa kesi 1 hadi 4, unaweza ombwa kurudisha thibitisho la ombi la hifadhi au ikose kurudiliwa na uamuriwe kuondoka nchini Ufaransa.

Ikiwa umelengwa na Amri ya Kuondoka Nchini Ufaransa (OQTF), unaweza pewa makazi ili upate matibabu kwa haraka na hati yako ya ombi la hifadhi ifuatiwe kwa haraka au utiwe kizuizini ikiwa ni lazima ili kuthibitisha madhumuni ya ombi lako au ikiwa usalama wa kitaifa au hali ya umma italazimisha kufanya hivyo.

Ikiwa rufaa haijasitisha mara moja, unaweza hata hivyo omba mahakama ya utawala, kwa hali ya hati dhidi ya OQTF iliyo kulenga, kusitishwa kwa amri ya kizuizi ili ufanye rufaa mbele ya CNDA dhidi ya maamuzi ya OFPRA, na pia ili CNDA ipate muda wa kufanya maamuzi juu ya kesi yako ikiwa watatakiwa kufanya hivyo.

Kumbuka kwamba, OQTF iliyochukuliwa baada ya maamuzi ya kukataa ombi la hifadhi inaweza pingwa mbele ya mahakama ya utawala kwa muda wa siku kumi na tano baada ya maarifa. Hakimu atafanya maamuzi kwa muda wa wiki kumi. Muda wa rufaa inafupishwa hadi saa 48 ikiwa umepewa makazi au umewekwa kizuizini. Katika tukio hili, hakimu anafanya maamuzi kwa muda wa saa 72.

